# MAPENDEKEZO YA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

# RIPOTI YA UTAFITI WA ENEO LA UWAJIBIKAJI KWA JAMII

## RIPOTI NAMBA 13 /2022

**09 SEPTEMBA, 2022**

**MHESHIMIWA HAROUN ALI SULEIMAN,**

**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS- KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA,**

**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA DKT. MWINYI TALIB HAJI,**

**MWANASHERIA MKUU WA ZANZIBAR,**

**ZANZIBAR.**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya Mwaka 1986, kwa heshima, Tume inawasilisha Ripoti ya Utafiti wa Eneo la Uwajibikaji kwa Jamii Zanzibar.

**…………..…………..**

**KHADIJA SHAMTE MZEE**
**MWENYEKITI,**
**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA,**
**ZANZIBAR**

**09 SEPTEMBA, 2022.**

# MAKAMISHNA WA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR



**ND. KHADIJA SHAMTE MZEE**
**MWENYEKITI**



**DKT.YAHYA KHAMIS HAMAD**
**KAMISHNA**



**ND. SALIM MOHAMED ABDALLA**
**KAMISHNA**



**ND. JUMA MSAFIRI KARIBONA**
**KAMISHNA**



**DKT. SIKUJUA OMAR HAMDAN**
**KAMISHNA**



**MHE. JAJI AZIZA IDDI SUWEDI**
**KAMISHNA**



**ND. MUSSA KOMBO BAKARI**
**KATIBU**

| | |
|---|---|
| Nd. Khadija Shamte Mzee | Mwenyekiti |
| Mhe. Jaji Aziza Iddi Suwedi | Kamishna |
| Dkt. Yahya Khamis Hamad | Kamishna |
| Dkt. Sikujuwa Omar Hamdan | Kamishna |
| Nd. Salum Mohammed Abdalla | Kamishna |
| Nd. Juma Msafiri Karibona | Kamishna |
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu |

**WATAFITI**

| | |
|---|---|
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu wa Tume |
| Dkt Mahfoudha Masoud | Mtafiti wa Sheria |
| Nd. Khamis Ali Jaku | Mtafiti wa Sheria |

Tume ya Kurekebisha Sheria

Vuga, Zanzibar-

P.O BOX 2539,

Simu +255 24 2231143,

Nukushi +255 24 2231137,

barua pepe info@lrcz.go.tz,

tovuti www.lrcz.go.tz

## YALIYOMO

**Makamishna……………………………………………………………………………..ii**

**Yaliyomo…………………………………………………………………………………..iv**

**Orodha ya Sheria na Sera zilizotumika……………………………………………...vii**

**Shukrani…………………………………………………………………………………...x**

**Vifupisho vya Maneno…………………………………………………………………..xii**

**Muhtasari………………………………………………………………………………...xiii**

**SURA YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI…………………………………………………………………………….1**

**1.1 Mamlaka ya Tume…………………………………………………………………….1**

1.2 Historia ya Uwajibikaji wa Wawekezaji duniani………………………………………………...2

1.3 Chimbuko la utafiti…………………………………………………………………………………..6

1.4 Maelezo ya tatizo……………………………………………………………………………………...7

1.5 Malengo ya utafiti……………………………………………………………………………………..7

1.6 Hadidu reje…………………………………………………………………………………………….7

1.7 Njia za kufanya utafiti……………………………………………………………………………….8

**SURA YA PILI**

**2.0 DHANA YA UWAJIBIKAJI KWA JAMAA……………………………………………………9**

**2.1 Maana ya Uwajibikaji kwa Jamii……………………………………………………………9**

2.2 Wajibu wa Wawekezaji, taasisis na kampuni katika CSR…………...............................10

2.3 Faida za CSR…………………………………………………………………………………………..13

2.4 Htua za kuchukuliwa katika CSR…………………………………………………………………..14

2.5 Changamoto katika utekelezaji wa miradi ya CSR…………………………………………….15

**SURA YA TATU**

**3.0 UCHAMBUZI WA SERA NA MFUMO WA KISHERIA……………………………………17**

**3.1 Utangulizi………………………………………………………………………………………...17**

3.2 Miongozo mikuu……………………………………………………………………………………...17

3.3 Sera……………………………………………………………………………………………………...20
3.4 Sheria ………………………………………………………..…………………………………………23

**SURA YA NNE**
**4.0 UTANGULIZI…………………………………………………………………………………………28**
**4.1 Makundi ya Waddau Walioshiriki na Taasisi Walizotoka…………………………...28**
4.2 Maoni ya Wadau………………………………………………………………………………….28
4.2.1 Maoni ya Kisheria…………………………………………………………………………...28

**SURA YA TANO**
**5.0 MIKATABA YA KIMATAIFA NA UZOEFU WA NCHI MBALIMBALI…………………..32**
**5.1 Utangulizi……………………………………………………………………………………….32**
5.2 Umoja wa Mataifa – UN……………………………………………………………………...33
5.3 OECD…………………………………………………………………………………………………35
5.4 Shirika la Kazi Duniani…………………………………………………………………….36
5.4.1 Azimio la Kanuni na Haki za Msingi Kazini……………………………………...38
5.42 Azimio la MNE……………………………………………………………………………….39
5.5 Umoja wa Ulaya na CSR…………………………………………………………………...40
5.5.1 Mkakati wa Ulaya wa kukuza CSR……………………………………………………41
5.6 Mkataba wa AFCFTA……………………………………………………………………...42
5.7 Agenda 2063 na biashara………………………………………………………………...43
5.8 Uzoefu wan chi mbali mbali…………………………………………………………….44
5.8.1 Tanzania………………………………………………………………………………………44
5.8.2 Kenya………………………………………………………………………………………...49
5.8.3 Uganda……………………………………………………………………………………….51
5.8.4 Philippines…………………………………………………………………………………53
5.8.5 Afrika Kusini……………………………………………………………………………...56
5.9 Hitimisho……………………………………………………………………………………….65

**SURA YA SITA**
**6.0 MATOKEO YA UTAFITI…………………………………………………………………...66**

**6.1 Njia zilizotumika katika Utafiti…………………………………………………………………....66**
6.2 Uchambuzi wa wadau…………………………………………………………………………..........66
6.3 Sampuli za utafiti……………………………………………………………………………………..67
6.4 Matokeo ya Utafiti…………………………………………………………………………………...74

**SURA YA SABA**
**7.0 MAPENDEKEZO YA TUME NA HITIMISHO…………………………………………………83**
**7.1 Utangulizi……………………………………………………………………………………………83**
7.2 Mapendekezo ya Kisheria…………………………………………………………………...........83
7.3 Mapendekezo ya Kiutendaji…………………………………………………………………...85
7.4 Hitimisho………………………………………………………………………………….............86
**7.5 Rejea………………………………………………………………………………………………....88**

## ORODHA YA SHERIA NA SERA ZILIZOTUMIKA

**Sheria Zanzibar**
sheria ya Utalii Nam. 9 ya mwaka 1996
Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar Nam. 16 ya mwaka 1986
Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984
Dira ya maendeleo 2050
Ilani ya CCM 2020-2025
Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011
Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2005
Sera ya Mazingira ya mwaka 2013
Sera ya PPP ya mwaka 2014
Sera ya Utalii ya mwaka 2017
Sera ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2016
Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar Nam. 14 ya Mwaka 2018
Sheria ya Mafuta na Gesi Zanzibar Nam. 6 ya mwaka 2016
Sheria ya Utalii Zanzibar Nam. 6 ya mwaka 2009
Sheria ya Kampuni Zanzibar Nam. 15 ya mwaka 2013
Sheria ya Mamlaka ya Bahari ya Nam. 3 ya mwaka 2009
Sheria ya PPP Nam. 8 ya mwaka 2015
Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Nam. 3 ya mwaka 2015
Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma Nam. 6 ya mwaka 2021

**Sera**
Zanzibar Development Vision 2050

The Zanzibar Strategy for Growth and Reduction of Poverty III. (MKUZA III)

Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025

Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011

Sera ya Utawala bora uk. 3, 4.

Sera ya Utawala bora uk. 5

Sera ya Uwekezaji 2005

The Zanzibar Environmental Policy 2013

Sera ya Mazingira 2013

Zanzibar Public Private Partnership Policy 2014

Sera ya Utalii ya mwaka 2017

**Sheria**

**Tanzania**

Sheria ya Kampuni Nam. 12 ya mwaka 2002 [Cap.212, R.E 2002]
Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Nam. 5 ya 1994
Sheria ya Ardhi ya Kijiji Nam. 5 ya mwaka 1999
Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Nam. 20 ya mwaka 2004
Sheria ya Petroli Nam. 8 ya mwaka 2015
Sheria ya Madini ya Tanzania Nam. 14 ya mwaka 2010

**Kenya**

Sheria ya Soko la Hisa (Sura 485A)
Sheria ya Kampuni ya 2009
CAP. 485A: Guidelines on Corporate Governance Practices by Public Listed Companies In Kenya. Gazette Notice No. 3362

**Uganda**

Sheria ya Kampuni, Sura ya 110 ya mwaka 2012
Sheria ya Mamlaka ya Soko la Mitaji ya 1996 Sura ya 84, R.E 2000
Capital Markets Corporate Governance Guidelines of 2003

**Philippines**

Sheria ya Uwajibikaji wa Wawekezaji kwa Jamii First Regular Session, SENATE S.B. No. 1239

An Act Institutionalizing Corporate Social Responsibility among Large Tax Payers and Providing Incentives Therefor 2747

**Afrika Kusini**

The South African Constitution, No 108 of 1996
The Broad-Based Black Economic Empowerment Act 2008
Sheria ya Kampuni Nam. 71 ya mwaka 2008
the Companies Amendment Act No.3 of 2011

The Employment Equity Amendment Act, No 47 of 2013 (EEA)
The King Reports – "Codex" ya CSR
the King Report on Corporate Governance ("King Report 1994") in 1994,
King Report on Corporate Governance for South Africa, 2002: *King Report on Corporate Governance for South Africa 2002*

**India**
Sheria ya Kampuni Nam. 18 ya mwaka 2013

**Indonesia**
Katiba ya Indonesia ya mwaka 1945, Undang-Undang Dasar 1945
the Indonesia's Limited Liability Company Act, Number 40 of 2007,
Sheria ya Mafuta na Gesi Nam. 22 ya mwaka 2001
Sheria ya Mashirika yanayomilikiwa na Serikali Nam. 19 ya mwaka 2003
Sheria ya Uwekezaji Nam. 25 ya mwaka 2007

## SHUKRANI

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imefanikiwa kukamilisha utafiti wa eneo hili la Uwajibikaji kwa Jamii unaopaswa kufanywa na wawekezaji, kampuni mbali mbali na taasisi nyengine zinazofanya biashara na kupata faida. Kazi hii ya utafiti imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na ushirikiano wa  wa taasisi na watu mbali mbali.

Shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia eneo hili na kutaka liwekewe utaratibu kwa lengo la kunufaisha jamii. Aidha shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Mwalim Haroun Ali Suleiman , Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa juhudi zake katika kusimamia utawala bora na kutaka sehemu hii ya uwajibikaji kwa jamii ambayo ipo katika misingi ya utawala bora ikamilishwe kwa kuwekewa sheria maalum.

Aidha, Tume inatoa shukrani kwa taasisi hizo zilizosaidia kukamilisha kazi ya utafiti huu. Tume inachukua nafasi hii kuwashkuru kwa dhati wote waliochangia katika kufanikisha utafiti huu. Ripoti hii inatambua baadhi ya taasisi hizo kutokana na michango yao kwa Tume wakati wote wa utafiti huu. Waliochangia kufanikiwa kwa utafiti huu ni pamoja na viongozi na watendaji wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa msaada mkubwa waliotupatia tangu hatua za awali hadi kukamilika kwa utafiti huu. Ofisi hii ya Rais imesaidia katika eneo la utaalamu na kuwezesha kufanyika vikao vya kukusanya maoni katika eneo hilo la uwajibikaji kwa jamii.

Aidha, Tume inazishukuru taasisi nyengine mbali mbali za Serikali zilizoshiriki katika vikao mbali mbali vya kukusanya maoni kuhusiana na eneo hili. Taasisi hizo zilitoa michango yao ambayo imewezesha kwa kiasi kikubwa kuifanya ripoti hii kukamilika kwa ufanisi mkubwa. Taasisi hizo ni pamoja na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, Baraza la Manispaa Magharibi A, Baraza la Manispaa Magharibi B, Baraza la Manispaa Mjini, Baraza la Mji Kaskazini A, Baraza la Mji Kaskazini B, Halmashauri Wilaya ya Kusini, Halmashauri Wilaya ya Kati na Masheha na madiwani.

Mbali ya taasisi hizi za Serikali, Tume pia inazishukuru taasisi binafsi na jumuiya mbali mbali ambazo nazo zilisaidia kwa kiasi kikubwa kufanikisha utafiti huu kwa kutoa michango yao katika eneo hili. Taasisi hizo zinajumuisha Chama cha Mahoteli, Chama cha Wafanya biashara, Jumuiya ya Uwekezaji Sekta ya Utalii Zanzibar na Jumuiya ya watembeza wageni Zanzibar.

Tume inayashkuru makundi yote haya kwa michango yao hiyo ambayo imeimarisha kwa kiwango kikubwa utafiti huu na hatimaye kutayarisha ripoti hii. Tunawashkuru sana.

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| AfCTA | Agreement Establishing the African Continental Free Trade Area |
| BBBEE | the Broad-Based Black Economic Empowerment Act |
| CMA | the Capital Market Act |
| CSR | Corporate Social Responsibity |
| GRI | Global Reporting Initiative |
| EIA | Environmental Impact Assessment |
| EABC | East Africa Business Council |
| EMP | Environmental Management Programme |
| EMA | the Environmental Management Act |
| EEA | The Employment Equity Act |
| EIS | Environmental Information System |
| E.U | European Union |
| GRI | the Global Reporting Initiative |
| ICSR | International Corporate Social Responsibity |
| ILO | the International Labour Organization |
| ISO | International Organisation for Standardization |
| MNE | the Multinational Enterprises |
| NGOs | Non Governmental organizations |
| OECD | the Organization for Economic Co-operation and Development |
| PPP | Public Private Partnership |
| SDGs | Sustainable Development Goals |
| SMEs | Small and medium Enterprises |
| SOC | State Owned Corporation |
| SEC | Social and Ethical Committe |
| SMEs | Small and Medium Enterprises |
| TRBN | Tanzania Responsible Business Network |
| TPSF | Tanzania Private Sector Foundation |
| TNBC | Tanzania National Business Council |
| TCCIA | Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture |
| TIC | Tanzania Investment Centre |
| UN | United Nations |
| UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| WBCSD | World Business Council for Sustainable Development |

# MUHTASARI

CSR ni eneo muhimu na la kuzingatiwa katika maendeleo ya jamii na nchi kwa ujumla. Eneo hili awali lilitoa fursa za kutekeleza kwa hiari uwajibikaji kwa jamii. Lakini kwa sasa Serikali nyingi zinaongeza masuala ya CSR katika Sera za nchi, sera za biashara na uwekezaji na sheria.

Katika miaka ya karibuni, wigo wa kujumuisha CSR katika taratibu za kisheria na masuala ya maendeleo ya kiuchumi, kitamaduni, taaluma, mazingira, kazi, na kadhalika umeongezeka. Hata hivyo, wigo huu bado ni mdogo katika sera, sheria, mikataba ya biashara na uwekezaji na kampuni zinazotengeneza faida.

Kampuni, Mashirika, wawekezaji na wadau wengine wana jukumu la kutekeleza CSR kutokana na athari za miradi au shughuli zao katika jamii, kutangaza biashara zao, na kujenga imani kwa jamii inayowazunguka.

Kwa Zanzibar bado ujumuishwaji wa dhana ya CSR haujafikia hatua kubwa ikilinganishwa na nchi nyengine, na hivyo kuna haja ya kujumuishwa kwa dhana ya CSR katika sheria, sera, mikataba ya biashara na uwekezaji, uendeshaji wa mashirika ya umma na kampuni ili kuimarisha maslahi ya wananchi na kuwawezesha kukabiliana na baadhi ya changamoto za kiuchumi na kimaendeleo katika maeneo wanayoishi ambayo taasisi hizo zInaendesha shughuli zake.

Ujumuishaji wa vifungu vya CSR katika mikataba ya uwekezaji na kampuni pamoja na uanzishwaji wa sheria maalum ni njia ya kukabiliana na mapungufu yaliyopo katika haki na wajibu kwa biashara; na njia ya kutambua jukumu la biashara binafsi katika kukuza na kuendeleza haki za raia, wadau, wafanyakazi, na wengineo.

Utafiti huu umezingatia uzoefu wa nchi mbalimbali, mikataba ya kimataifa, sera na sheria zilizopo Zanzibar ambazo kwa kiasi kikubwa zimezingatia eneo la CSR. Tatizo lililobainika ni kutokuwepo uratibu wa utekelezaji wa shughuli za CSR, kuwepo kwa masharti na mifumo tofauti ya utekelezaji wa CSR, utofauti wa vipimo vinavyozingatiwa katika CSR, kutokuwekwa wazi wajibu, usahihi na tathmini au njia za utekelezaji wa vifungu vya CSR katika sheria na mikataba ya biashara na uwekezaji.

Utafiti huu umefafanua na kupendekeza uwepo wa sheria maalum ya kusimamia utekelezaji wa wajibu kwa jamii (CSR) katika nyanja zote pamoja na kufanya tathmini ya CSR kwa kampuni, wawekezaji na mashirika yaliyopo Zanzibar. Aidha, utafiti huu umependekeza kutolewa elimu ya kutosha kwa wananchi na wawekezaji ili wafahamu dhana ya CSR na jinsi inavyotakiwa kuwafaidisha, misingi yake pamoja na haki na wajibu wa wawekezaji, kampuni na taasisi zinazohusika.

Hata hivyo, Serikali nayo katika ngazi mbalimbali inatakiwa kutimiza ahadi zake hasa pale panapohitajika mashirikiano au nguvu za pamoja au kutekeleza CSR kwa kuzingatia makubaliano ambayo yanaweza kutoa mbinu za ziada za utekelezaji wake kwa faida ya biashara yenyewe na wananchi kwa ujumla.

Hivyo, utafiti huu umeainisha mapendekezo mbali mbali na maeneo ya kuzingatiwa katika sheria kama misingi ya CSR, usimamizi wake, taasisi zinazohusika, viwango vya uchangiaji, maeneo ya kujumuishwa katika CSR, Wajibu wa Serikali na taasisi zake, wajibu wa kampuni, taasisi na wawekezaji na uwajibikaji katika miradi na huduma za CSR

## SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Mamlaka ya Tume

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ni Taasisi ya kiserikali ambayo ipo chini ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imeanzishwa na Sheriaya Tume ya Kurekebisha Sheria ya Zanzibar Nam. 16 ya mwaka 1986.[1] Kwa mujibu wa Sheria hii Tume imepewa jukumu la kufanya tafiti na mapitio ya Sheria zote za Zanzibar,[2] kwa lengo la kupendekeza sheria mpya[3] au kuzirekebisha pale inapobidi ili zilingane na muelekeo wa mabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kwa watu wa Zanzibar.

Katika kutekeleza matakwa ya Sheria hii, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar hufanya tafiti za Sheria mbali mbali ili kuona kwamba ipo haja ya kutungwa sheria mpya, kufanyiwa marekebisho ya sheria, kufutwa au kuendelea kutumika kwa Sheria kulingana na mahitaji ya wazanzibari wote. Katika ufanyaji huo wa tafiti au mapitio ya Sheria, Tume hupokea ombi kutoka Serikalini, kutoka kwa wadau wa Sheria husika au Tume kuchukua maamuzi yenyewe katika kuangalia eneo gani linahitaji kufanyiwa utafiti au kufanya mapitio ya Sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho.

---

[1] Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar nambari 16 ya 1986
[2] Ibid Kifungu cha 4(1)
[3] Ibid Kifungu cha 4(2) (c) Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar

Hivyo, kupitia ripoti hii, Tume imefanya Utafiti wa Kisheria kuhusiana na Uwajibikaji kwa Jamii kwa lengo la kutoa mapendekezo ya kisheria na kiutendaji na kuisaidia Serikali katika kukamilisha malengo yake na maendeleo ya kijamii kwa ujumla.

## 1.2 Historia ya Uwajibikaji wa Wawekezaji duniani

CSR ni dhana ya muda mrefu ingawa imeshuhudiwa kuibuka baada ya Vita vya Pili vya Dunia, kwa taaluma ya masomo ya maendeleo na mabadiliko kadhaa ya kinadharia katika kuzingatia katika dhana ya maendeleo, na tafiti za maendeleo zimekuwa na uhusiano wa karibu zaidi na sera ya maendeleo na mambo yaliyokuwa yamezoeleka.[4]

Hata hivyo katika Karne ya 21, CSR imekuwa moja ya mada yenye ushawishi mkubwa ulimwenguni, katika masuala ya ajira, kitaaluma na katika maendeleo ya maisha ya kila siku,[5] na hivyo CSR imekuwa ni sehemu ya msamiati na ajenda katika nyanja zote za maisha, kutoka kwa wasomi hadi wataalamu, NGOs hadi vikundi vya watumiaji, wafanyakazi hadi wauzaji, wanahisa na wawekezaji.[6]

Katika mwaka 1998, Baraza la Biashara Ulimwenguni la Maendeleo Endelevu (WBCSD) lilifanya mazungumzo na wadau mbalimbali duniani kote imebaini

[4] OECD. 2000. Working Party of the Trade Committee, Codes of Corporate Conduct: An Expanded Review of their Contents. OECD Doc. TD/TC/WP(99)56/FINAL.

[5] Rafael Peels, Elizabeth Echeverria M., Jonas Aissi and Anselm Schneider, ILO Research Paper No. 13 Corporate Social Responsibility in International Trade and Investment Agreements: Implications for states, business and workers April 2016 International Labour Office

[6] Kashyap, Rajiv, Raza Mir and Ali Mir. 2003. Corporate Social Responsibility: A Call for Multidisciplinary Inquiry. Journal of Business & Economics Research 2(7): 51–58

kuwa CSR ina maana pana, kulingana na mambo ya ndani ikiwa ni pamoja na utamaduni, dini, na hali ya kiserikali au ya kisheria.[7]

Katika nchi nyingi za Afrika, CSR ilionekana zaidi kama njia ya kampuni kujihusisha na mambo ya mazingira ya kukuza uhusiano kati ya mikakati ya biashara na wadau wa kijamii na mikakati imezidi katika masoko na upatikanaji mapato.[8] Sera zisizo wazi zimeathiri kwa kuruhusu baadhi ya kampuni kuchukua fursa za biashara, na kutangaza bidhaa za kampuni kupitia mgongo wa CSR.[9]

Kwa upande wa Tanzania, kampuni nyingi za kigeni katika sekta ya benki, mawasiliano ya simu na madini zimekuwa zikifanya kazi za kuwajibika kwa jamii CSR. Mwaka 2010 na 2012, Benki kwa kushirikiana na Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC) ilianzisha na kufadhili Tuzo za CSR za Afrika Mashariki ili kutambua kampuni zinazofanya vizuri katika nyanja mbalimbali za uwajibikaji kwa Jamii.[10] Mpango huo ulibuniwa na kuratibiwa na Africapractice, ambayo ilifanya kazi ya utangazaji na kuhamasisha juu ya CSR kwa Tanzania.[11]

Kampuni za Kimataifa za Ukaguzi, Kodi na Uhasibu kama vile Deloitte, KPMG, na PWC walifanya CSR kuwa kwenye ajenda zao na kufikiria kutoa huduma

[7] WBCSD, 2015 World Business Council for Sustainable Development
[8] Lungu, John and Sumbye Kapena. 2010. South African mining companies in Southern Africa: corporate governance and corporate social responsibility. Johannesburg: South Africa resource watch, ukurssa wa 107
[9] Vertigans, S, et al (2016). Corporate Social Responsibility in Sub Saharan Africa; Sustainable development in its embryonic form; Sprinter, Switzerland. Page 114
[10] Chikati, John. 2010. Corporate Social Responsibility in Africa. Nairobi: REPARED Publishing Department.
[11] Corporate Social Responsibility in Tanzania: An Overview by Karin Mader CSR advisor and certified sustainability reporter Dar es Salaam, June 2012, ukurasa wa 5
https://csroverviewtanzania.files.wordpress.com/2012/08/csr-overview-tanzania3.pdf. Ukurasa wa 6

katika eneo la Tanzania. Mtandao wa Biashara Wanaojibika Tanzania (TRBN) unaunganisha kampuni na kuzingatia kuzingatia uendelevu na maadili ya biashara, hasa kutetea mipango ya kupambana na ufisadi katika sekta ya kibinafsi ya nchi.[12]

Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ni mpango wa sekta binafsi katika kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi yanayoongozwa na sekta binafsi nchini Tanzania kwa kuzingatia sera na kujenga uwezo. Ikiungwa mkono na wafadhili kadhaa wa kimataifa, TPSF inafanya kazi kwa karibu na Baraza la Taifa la Biashara Tanzania (TNBC). Idadi ya mashirika mwamvuli ya viwanda yapo nchini Tanzania, kama vile jumuiya ya ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) inayoendesha ofisi katika mikoa na wilaya nyingi nchini kutoa ushauri wa kibiashara, maendeleo na huduma za upatanishi katika ngazi ya mtaa.[13]

Kutokana na hatua hii Serikali pia imeweka Sera, sheria na miongozo mbalimbali katika maeneo yanayohusiana na CSR kama vile sera za uhifadhi wa mazingira, kanuni kuhusu VVU/UKIMWI, Sheria ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi n.k. Tanzania imeridhia idadi ya mikataba ya kimataifa inayohusu Haki za Binadamu, Mabadiliko ya Tabianchi, Kupambana na Ufisadi na maeneo mengine yanayohusiana na CSR. Ufafanuzi wa uwazi na kanuni maalum kuhusu Biashara na uwajibikaji kwa Jamii.[14] Baraza la Taifa la Biashara Tanzania (TNBC) ndilo jukwaa rasmi la mashauriano kati ya sekta ya umma na

[12] ibid ukurasa wa 6
[13] Lunogelo, Bohela and Apronius V. Mbilinyi. 2009. Convergence of COMESA-SADC-EAC Regional Frameworks. A Paper Presented During the Annual Forum for Private, Public and Academia Partnership on Trade Policy and Negotiations and organized by the Ministry of Industry, Trade and Marketing (MITM) in 26th October, 2009.
[14] Corporate Social Responsibility in Tanzania: Experience of Misconception, Misuse and Malpractices Shukrani K. Mbirigenda

sekta binafsi, linaloongozwa na Rais wa Tanzania. Baraza hilo lina wawakilishi 40, 20 kutoka sekta binafsi na 20 kutoka Serikalini na wataalam.[15]

Aidha Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ndicho wakala wa msingi wa Serikali kukuza na kuwezesha uwekezaji nchini na kuishauri Serikali mambo yanayohusiana na uwekezaji. TIC pia imepewa jukumu la kuratibu miradi ndani ya upeo wa Sheria ya Ushirikiano wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, na inahimiza sekta ya biashara kuwa mshirika wa maendeleo wa nchi, na kuunga mkono malengo ya maendeleo ya nchi, kwa upande mwengine.

Hata hivyo wakati mwengine kampuni nchini Tanzania haikuweza kuzingatia hata kanuni za kawaida za biashara. Isipokuwa baadhi kufanya aina za ujanja wa kuchangia ili kuonekana safi na kusifiwa katika kulipa kodi zao na kuchangia maendeleo ya jamii, huku kiutendaji kampuni hizi zikikwepa mambo ya msingi.[16]

Kwa Zanzibar dhana ya CSR imezingatiwa katika sheria mbalimbali tokea wakati wa ukoloni kwa kuweka baadhi ya vifungu vya uwazi na uwajibikaji katika sheria ya Kampuni Sura ya 153. Sheria hii ililazimisha Kampuni kuwasilisha taarifa zao za mapato na uwajibikaji kila mwaka.

---

[15] CONTEMPORARY CONCERNS IN DEVELOPMENT STUDIES: PERSPECTIVES FROM TANZANIA AND ZAMBIA, Edited by Rehema Kilonzo & Tiina Kontinen, file:///C:/Users/HP/Downloads/Mbirigenda-Contemproraryconcernsindevelopmentstudies.pdf Publications of the Department of Political and Economic Studies 23 (2015) Development Studies, University of Helsinki, Finland

[16] Egels, Niklas. 2005. CSR in Electrification of Rural Africa: The Case of ABB in Tanzania. Goteborg: Greenleaf Publication. Uk 108

Aidha katika miaka ya 1990 wakati wa mabadiliko ya uchumi, Zanzibar ilipitisha sheria mmbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa hazikueleza moja kwa moja lakini ziligusa misingi na dhana ya uwajibikaji kwa jamii. Sheria zilizopitishwa kipindi hico ni Pamoja na Sheria ya usimamizi wa Mazingira Nam. 2 ya mwaka 1996 ambayo ilieleza misingi ya tathmini ya mazingira na taratibu zake na kubainisha wazi wajibu wa wawekezaji na kampuni kuzingatia misingi ya EIA na kuwa na mifumo ya EIS katikashughuli zao ili kulinda mazingira na kuwa na maslahi ya uchumi wa taifa,[17] aidha sheria hii katika kifungu cha 86 imeeleza kulindwa kwa baianuwai na kuhakikisha kampuni na wawekezaji wanazingatia ulinzi mzuri wa mazingira.

Sheria nyengine ambayo ilihusika na CSR ni Sheria ya. Uwekezaji Nam. 11 ya mwaka 2004 ambayo katika kifungu cha 11(4) ilieleza umuhimu wa wawekezaji kuzingatia maslahi ya nchi na kuhakikisha wananchi wanafaidika na uwekezaji katika maeneo waliyopo.

Sheria ya Kuimarisha Utalii nayo haikueleza kwa uwazi eneo la CSR ingawa kuna vifungu vya adhabu mbavyo vinaeleza kuwa ni kosa kwa kapuni au hoteli kukiuka sheria nyengine, na kufanya biashara kinyume na maslahi ya umma, misingi ya utalii na maslahi ya wananchi.[18]

Maendeleo ya kuzingatia eneo la uwajibikaji kwa jamii CSR liliwekwa vizuri zaidi katika miaka ya 2000 kwa kujumuisha taasisi binafsi, kampuni, wawekezaji na mashirika ya umma, kwa kufuta sheria na kupitisha sheria mpya

---

[17] Sehemu ya VII, kifungu cha 38-62

[18] Kifungu cha 9(2)(b) na (d), sheria ya utalii Nam. 9 ya mwaka 1996.

zilizozingatia dhana ya CSR kama sheria ya ZIPA Nam. 14 ya 2018, Mafuta na Sheria ya Mafuta na Gesi Nam. 6 ya 2016, sheria ya Utalii Nam. 6 ya 2009, Sheria ya Kampuni nam. 15 ya 2013, Sheria ya PPP Nam. 8 ya 2015, Sheria ya mazingira Nam. 3 ya 2015 na Msajili wa Hazina Nam. 6 ya 2021. Mbali ya uwepo wa sheria hizo, kuna baadhi ya taasisi, kampuni, wawekezaji, Asasi za kiraia ambazo zimekuwa zikisaidia jamii na kuwajibika katika miradi, misaada na huduma mbalimbali kwa wananchi wa Zanzibar.

### 1.3 Chimbuko la utafiti

Chimbuko la utafiti huu ni dhamira ya Serikali kuanzisha utaratibu wa kisheria kwa upande wa usimamizi wa utekelezaji wa wajibu wa Wawekezaji kwa Jamii ili kuleta mageuzi makubwa ya kimaendeleo kwa upande wa Serikali. Aidha utafiti huu umechangiwa pia na utekelezaji wa Sera ya utawala Bora ambayo kwa kiasi kikubwa imegusa eneo hili na kutaka kampuni, wawekezaji, taasisi zenye faida kuwajibika kwa jamii katika maeneo waliopo.

### 1.4 Maelezo ya tatizo.

Uwajibikaji wa Wawekezaji kwa Jamii (CSR) ni dhana iliyokuwa sana kwa sasa na inachangia kwa kiasi kikubwa manedeleo ya haraka na kusaidia utekelezaji wa mipango ya nchi. Dhana hii kwa Zanzibar imeelezwa katika sheria mbalimbali na kwa utaratibu tafauti hali inayofanya kutokuwepo usawa katika usimamizi na utekelezaji wake. Hivyo Serikali imeona kuna haja ya kuwa na utaratibu maalum wa kusimamia utekelezaji mzima wa Wajibu wa Wawekezaji kwa Jamii na mambo yanayohusiana ili kuhakikisha wawekezaji, kampuni, mashirika yanayotengeneza faida, Asasi za kiraia n.k kutekelza wajibu wa o wa kusaidia jamii katika misingi na utaratibu unaofahamika kisheria.

## 1.5 Malengo ya utafiti

Malengo ya utafiti huu ni kuangalia utaratibu unaotakiwa katika usimamizi wa CSR, kutathminin sheria na taratibu zilizopo Zanzibar na kutoa mapendekezo ya kisheria pamoja na kiutendaji ikiwemo uanzishwaji wa Sheria maalum ya kusimamia suala zima la wajibu wa uwajibikaji kwa jamii.

## 1.6 Hadidu rejea

Katika kufanya utafiti huu Hadidu Rejea zifuatazo zilizingatiwa:

(a) Kufanya utafiti wa kina kwa lengo la kujua dhana nzima ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR)

(b) Kuangalia uzoefu wa Sheria za nchi mbali mbali kuhusiana na suala CSR na kuangalia namna uzoefu huo huo unavyoweza kutumika kwa mazingira ya Zanzibar;

(c) Kuangalia Sera na Sheria mbali mbali za Zanzibar na mikataba inayoelezea usimamizi wa wawekezaji na uwekezaji kwa ujumla hususani katika suala la uwajibikaji kwa jamii;

(d) Kuchukua maoni ya wadau muhimu kuhusiana na utafiti huu kwa lengo la kutoa mapendekezo juu ya sheria ya kusimamia wajibu wa Kuwajibika kwa wananchi.

## 1.7 Njia za kufanya utafiti.

Katika kufanya utafiti huu, njia mbalimbali zimetumika ikiwemo kupitia rejea mbali mbali za ndani na nje ya nchi, na kuangalia miongozo ya kimataifa na sheria za nchi nyengine, Katiba, Sera na Sheria mbali mbali, pamoja na

kukusanya maoni ya wadau na washiriki wakubwa wa dhana ya uwajibikaji kwa jamii.

# SURA YA PILI

## 2.0 DHANA YA UWAJIBIKAJI KWA JAMII

### 2.1 Maana ya Uwajibikaji kwa Jamii

CSR ni dhana isiyo na ufafanuzi wa moja kwa moja uliokubaliwa kwa wote,[19] hata hivyo, katika moja ya tafsiri iliyotolewa ni kampuni kuzingatia na kufanyiakazi mahitaji ya kiuchumi, kitaalam na kisheria ili kutimiza faida za kijamii pamoja na faida za kiuchumi kwa jamii.[20]

Kwa urahisi, CSR inaweza kufafanuliwa kama taasisi au kampuni inayofanya kazi kwa njia endelevu ya kiuchumi, kijamii na kimazingira na ni dhana ambayo inatarajia bodi za mashirika na kampuni kuzingatia, kudhibiti na kusawazisha athari za kiuchumi, kijamii na kimazingira za shughuli zao.[21]

Dhana ya CSR inategemea kanuni za kampuni au taasisi, na uendelevu wa mazingira katika jamii. Ili jamii iweze kupata maendeleo, taasisi nan kampuni

[19] Dahlsrud, A. (2008) How Corporate Social Responsibility Is Defined: An Analysis of 37 Definitions. Corporate Social Responsibility and Environmental Management, 15, 1-13. http://dx.doi.org/10.1002/csr.132

[20] Davis, K. (1973) The Case for and against Business Assumption of Social Responsibilities. Academy of Management Journal, 16, 312-322. http://dx.doi.org/10.2307/255331

[21] Félix-Fernando Muñoz, María-Isabel Encinar, Carolina Cañibano (2012) "On Economics, Ethics, and Corporate Social Responsibility" Modern Economy Vol.3 No.4, July 24,2012 DOI: 10.4236/me.2012.34046

zenye faida na ushindani ni muhimu kusaidia katika maeneo ya ajira, miradi na huduma za kijamii.[22]

Shirika la Kimataifa la Viwango (ISO) linatumia neno uwajibikaji wa shirika au Kampuni na linatoa ufafanuzi kwamba Wajibu kwa kijamii ni wajibu wa shirika kwa athari kwa maamuzi na shughuli zake kwa jamii na mazingira, kupitia uwazi na maadili, matarajio ya wanahisa; kutii sheria inayotumika na inalingana na kanuni za tabia za kimataifa; na kuendeleza uhusiano wake.[23] Tafsiri nyengine iliyokubaliwa ni hali ya wawekezaji au kampuni kuchangia katika maendeleo, hasa ya kiuchumi na kijamii katika jamii inayoizunguka, yakisaidia kuimarisha maisha ya wafanyakazi na jamii nzima kwa ujumla.[24]

Kutokana na hayo yaliyotangulia, ni wazi kwamba neno uwajibikaji wa jamii kwa Kampuni au shirika linajumuisha sio tu kutii wajibu wa kisheria wa kampuni au taasisi, sheria ya mazingira na kazi, lakini pia kujitolea kwa hiari kwa mazoea ya kimaadili na uendelevu ambayo yananufaisha jamii na mafanikio ya muda mrefu.[25]

## 2.2 Wajibu wa Wawekezaji, taasisi na kampuni katika CSR

[22] Corporate Social Responsibility in Tanzania: An Overview by Karin Mader CSR advisor and certified sustainability reporter
Dar es Salaam, June 2012, ukurasa wa 4
https://csroverviewtanzania.files.wordpress.com/2012/08/csr-overview-tanzania3.pdf

[23] ISO Guidance on Social Responsibility : ISO 26000:2010(en) inapatikana https://www.iso.org/obp/ui/#iso:std:iso:26000:ed-1:v1:en

[24] Frederick, W.C. (2018), "Corporate Social Responsibility: From Founders to Millennials", *Corporate Social Responsibility* (*Business and Society 360, Vol. 2*), Emerald Publishing Limited, Bingley, pp. 3-38. https://doi.org/10.1108/S2514-175920180000002001

[25] Klettner, A. (2016). Corporate Governance Regulation: The Changing Roles and Responsibilities of Boards of Directors. London: Routledge.

Wajibu wa Kampuni au taasisi kwa Jamii (CSR) kwa miongo kadhaa imeonekana umuhimu wake ndani ya nchi, kikanda na kimataifa. Kampuni kubwa huchukua fursa na kuamua kutumika kama watoa huduma na idadi ya shughuli nyingi zinafanyika kusaidia jamii inayowazunguka.[26]

Wajibu wa Uwajibikaji kwa Jamii ni njia mojawapo ya kuimarisha mahusiano kati ya Wawekezaji na jamii inayoizunguka, na kuna faida nyingi kwa Wawekezaji, ikiwemo kuwaletea Wawekezaji hao faida nzuri, kuongeza uwezekano wa kubakisha wafanyakazi na kuyafanya Wawekezaji hao wakubalike katika jamii.[27]

Jukumu la CSR kwa biashara na kwa jamii ni muhimu zaidi, CSR inahusu kujitolea kwa biashara kwa mojawapo ya maeneo yaliyotajwa bila kuwa na hitaji au usalama wa faida kwenye uwekezaji.[28] Mapambano mara nyingi huwa katika kutambua maeneo ambayo yanafaa zaidi kwa biashara na kukubali kwamba ni vigumu kupima kwa usahihi athari za ushiriki wa taasisi au kampuni.[29]

Kimsingi kuna fursa nyingi na nafasi kubwa ya ukuaji uchumi kama vile huduma za afya, elimu, kijamii, miundombinu, uundaji wa nafasi za kazi na mazingira yanahitaji ushiriki wa CSR na maendeleo ambayo yatasaidia sana

[26] Vergalli, (2009,August) Does Corporate Social Responsibility Affect the Performance of Firms? (August , 2009). FEEM Working Paper No. 52.2009.
[27] Fundikila wazambi & joice komanya, muhtasari wa ripoti ya haki za binaadamu na biashara, octoba 2019.
[28] Amponsah-Tawiah, K., & Dartey-Baah, K. (2011) "Corporate Social Responsibility in Ghana. International" Journal of Business and Social Science, 2, 107-112.
[29] Brummer, J.J. (1991) "Corporate Responsibility and legitimacy: An interdisciplinary analysis." Wesport CT: Greenwood press

kuhudumia jamii kwa njia yenye matokeo.[30] Juhudi hizi hazisukumwi tu na wafanyabiashara wanaoshiriki kwa hiari bali biashara zinazowawezesha wajasiriamali wa ndani na watu kuwa sehemu ya ukuaji na maendeleo ya jumuiya zao.[31]

Kulingana na Carroll (1999), wajibu wa jukumu kwa kijamii unazingatia viwango, kanuni, na matarajio ambayo yanaakisi kwamba Kampuni imeijali jamii, watumiaji, wafanyakazi, wanahisa, na wadau wengine na hii inakichukuliwa kama haki au kuzingatia heshima au ulinzi wa wanahisa wa kampuni husika.[32]

Horrigan anaeleza kwamba Kampuni zina wajibu wa kujitolea kwa CSR, na ni lazima wafanye hivyo kwa madhumuni ya kushirikiana na jamii na wadau wengine, kuweka uaminifu wa CSR, kupata fursa ya kushiriki ya kutowajibika kwa kampuni, kutoa ushawishi kwa sera ya umma ya CSR na maendeleo.[33]

Wajibu wa Wawekezaji ni mchakato unaohusika na kuwajibika kwa wahusika wa Kampuni au Taasisi kulingana na Kanuni za Kimataifa katika miongozo ya taratibu za kibiashara.[34] Wajibu unajumuisha kuhakikisha inaleta tija kwa wamiliki wake kupitia uingizaji wa faida na ukuaji kimasoko; Wateja

[30] Carroll, A. B. (1979). „A three- dimensional conceptual model of corporate social performance‟ Academy of Management Review, 4, 497-50

[31] Misbau Alamu Lateef, Adedoyin Olusegun Akinsulore (2021) "Covid-19: Implications for Corporate Governance and Corporate Social Responsibility (CSR) in Africa: Africa, Corporate Governance, CSR, COVID19" **Beijing Law Review**, Vol.12 No.1, March 16, 2021

[32] Archie B Carroll, (1999) "Corporate social responsibility: Evolution of a definitional construct" September 1999, Business & Society 38(3):268-295. University of Georgia

[33] Horrigan,B .(2010) "Corporate Social Responsibility in the 21st Century: Debates, Models and Practices Across Government, Law and Business;" Edward Elgar Publishing, 2010; Sdney

[34] Michael Hopkins: A Planetary Bargain: (2003) "Corporate Social Responsibility Comes of Age (Macmillan, UK, 1998;" updated and re-printed by Earthscan, 2003 and again reprinted by Routledge, UK

(Customers), kufanikiwa au kufeli kwa kampuni kwa kiasi kikubwa kupo mikononi mwa wateja wake. Kwa mantiki hii, ni wajibu wa kampuni kuhakikisha inawapatia wateja wake kile wanachohitaji.

Wajibu mwengine ni kwa wafanyakazi ambao ndio wazalishaji wa bidhaa na huduma za kampuni; Serikali kupitia kufuata taratibu na sheria zilizowekwa na mamlaka katika uendeshaji wa shughuli za kibiashara; jamii kwa kuchangia katika maendeleo na ustawi mzima wa jamii.[35]

## 2.3 Faida za CSR

CSR ina faida nyingi kwa biashara na Serikali ikiwemo uwajibikaji wa kijamii na kimaadili kwa biashara na kusaidia miundombinu ya kijamii ambayo inahusisha biashara kuchangia manufaa ya wote; na michango kwa mashirika ya kiraia ili kuhakikisha masharti ya kupata faida yenye mafanikio.[36]

Faida nyengine ni katika biashara ambapo mipango, miundo ya usimamizi na michakato ya ushiriki wa wadau kupitia mawasiliano mbalimbali yanaweza kufanywa kupitia CSR.[37] Aidha, CSR inatoa faida za ubia, mitandao na kujenga muungano kwa biashara. Hii ni pamoja na kukuza uhusiano, kuimarisha

[35] Kituo cha Sheria na Haki za Binaadamu, Muongoo wa Misingi ya Biashara na Haki za Binaaadamu: pub, 11/0$/2011

[36] Horrigan, B. (2010) "Corporate Social Responsibility in the 21st Century: Debates, Models and Practices Across Government, Law and Business;" Edward Elgar Publishing, 2010; Sdney ukurasa wa 271

[37] Ali, I., Rehman, K.U., Yilmaz, A.K., Nazir, S and Ali, J.F. (2010) "Effects of corporate social responsibility on consumer retention in cellular industry of Pakistan," African Journal of Business Management. Vol. 4(4), Pp. 475-485.

uaminifu na kushiriki kutoa utaalamu, faida za biashara kupitia ushiriki katika mipango ya mbalimbali kisekta.[38]

CSR, inasaidia kutumia masoko mapya na kuzalisha mapato ya kifedha kwa kuwajibika kijamii na kimazingira katika shughuli ya biashara. Hii inajumuisha njia ambazo CSR husaidia kukuza ushindani biashara.[39]

CSR inasaidia kutambuliwa aina za biashara au kampuni, na kuongeza faida kwa kampuni;[40] kuongezeka kwa mauzo na uaminifu wa wateja; uwezo mkubwa wa kuvutia vipaji na kubakiza wafanyakazi; ukuaji wa shirika na upatikanaji rahisi wa mtaji.

Mwisho, uwajibikaji wa jamii (CSR) huisaidia Serikali katika kutatua mahitaji mbalimbali ya kijamii ikiwemo masuala ya elimu, maji, masuala ya afya, miundombinu n.k; kukuza uchumi kwa kutoa nafasi za ubia, ajira na kujenga muunganiko wa kibiashara.[41]

## 2.4 Hatua za kuchukuliwa katika CSR

Kuna hatua mbalimbali za kuchukuliwa na Kampuni katika CSR ikiwemo kufanya uchunguzi wa awali wa ndani, kabla ya kutangaza hadharani kuhusu CSR. Kampuni zinapaswa kufanya uchunguzi ili kuepuka uharibifu wa sifa na

[38] Du, S., Bhattacharya, C. B. and Sen, S. (2010) “Maximising business returns to corporate social responsibility (CSR): The role of social responsibility communication”. International Journal of Management Reviews. Vol. 12(1), Pp. 8-19.

[39] Branco, M. C. and Rodrigues, L. L. (2006) “Corporate social responsibility and resource-based perspectives.” Journal of Business Ethics, Vol. 69, Pp. 111-132.

[40] Turban, D. B. and Cable, D. M. (2003) “Firm reputation and applicant pool characteristics.” Journal of Organisational Behaviour. Vol. 24 (6), Pp. 733-751.

[41] Mullerat Ramon (ed.) (2010) “Corporate Social Responsibility - The Corporate Governance of the 21st Century”, Kluwer Law International (revised edition, 2010)

dhima inayochukuliwa na taasisi au kampuni au madai yoyote kabla ya miradi kutekelezwa.[42]

Kwa mfano Tanzania kuna kampuni ambazo zimejaribu kujihusisha katika jamii kwa kusaidia sekta zenye uhitaji na zisizojiweza nchini katika nyanja za elimu, afya, michezo, jinsia na mazingira. Lengo kuu likiwa ni kuongeza kiwango cha maisha, baadhi ya juhudi zimeonekana kama vile uchunguzi wa saratani ya matiti unaotetewa na MEWATA ambao hatimaye ulipata usaidizi mkubwa kutoka kwa taasisi tofauti za kifedha kama Diamond Trust Benki, NBC na Benki ya Standard Charter.[43]

Aidha, kampuni zinatakiwa kueleza kanuni zao na kuwa na akaunti ya kujitolea mahususi kwa kampuni kwa CSR. Kampuni zinapaswa kufanya hivyo kwa madhumuni ya kuwaleta pamoja katika mazungumzo wawekezaji na wadau wengine juu ya masuala ya CSR, kuanzisha uaminifu wa CSR na wadau na kushiriki katika mijadala ya umma kuhusu kutowajibika kwa kampuni.[44]

Kwa upande wa Serikali, viongozi wa makampuni wanapaswa kushirikishwa katika majadiliano si tu kwa sababu kampuni zao zina msaada lakini pia ni umuhimu kujua mikakati yao na kuwajibika kijamii na kisiasa. Hatua hii inasaidia kutumia fursa muhimu za soko kwa kuangazia mahitaji ya kijamii

[42] Horrigan,B .(2010) "Corporate Social Responsibility in the 21st Century: Debates, Models and Practices Across Government," Law and Business; Edward Elgar Publishing, 2010; Sdney

[43] Materu,T.B (2013) "People's perception of Corporate Social Responsibility in Sugar Estate: A case of Tanganyika Planting Company;" M.A Dissertation, University of Dar es Salaam, unpublished at Pp. 24-25.

[44] Susan Njeri Wamitu (2014) "Corporate Social Responsibility: Intentions and Practice" Open Journal of Business and Management Vol.2 No.2, April 29, 2014. DOI 10.4236/ojbm.2014.22015

ambayo hayajafikiwa na kutoa upendeleo wa wananchi waliokosa huduma fulani.[45]

## 2.5 Changamoto katika utekelezaji wa miradi ya CSR

Kuna udhaifu na changamoto ambazo CSR inakumbana nazo na kusababisha utekelezaji mbaya wa miradi inayosimamiwa. changamoto ya kwanza ni utendaji mbaya ambapo misingi ya CSR kutokuwa wazi, na kupelekea ukiukwaji wa mambo mbalimbali. Ukiukwaji unaweza wakati mwengine kuwa na lengo, na wakati mwengine kutokujua CSR inahusika na nini.[46]

Changamoto ya pili ni suala la sera za CSR ambazo baadhi hazipo na baadhi hazina uhakika. Hali hii inatoa mwanya wa matumizi mabaya ya utaratibu huu kwa Kampuni ambazo hutumia udhaifu huo kwa manufaa yao wenyewe, ikiwemo utangazaji wa chapa au utangazaji wa bidhaa, na kutumia CSR kimkakati kupata uungwaji mkono wa umma kwa uwepo wao katika masoko.[47]

Changamoto nyengine zinahusisha ubadhirifu wa fedha za miradi inayofadhiliwa hasa pale wakandarasi wa ndani wanapoajiriwa;[48] kutokutolewa michango kutoka katika Wilaya au taasisi ambazo zinatakiwa

---

[45] DENNIS C. LEKA REG. NO: LLM/CL/0004/T.14 "The Role of Corporate Social Responsibility in Achieving the Corporate Objectives: A Case Study of Songas" A Dissertation submitted to the Faculty of Law in Partial Fulfillment of the Requirements for the Award of the Degree of Masters of Laws (LL.M Commercial Law) of Mzumbe University. Ukursa wa 28-29. Inapatikana http://scholar.mzumbe.ac.tz/bitstream/handle/11192/2143/LLM-CL-LEKA-DENIS-2016.pdf?sequence=1

[46] Mbirigenda,S. (2015) "Corporate Social Responsibility in Tanzania: Experience of Misconception, Misuse and Malpractices," ukurasa wa 105

[47] Mader Karin, (2012) "Corporate Social Responsibility in Tanzania; An overview;" Dar es Salaam, ukurasa wa 7

[48] Robins, F. (2008) "Why corporate social responsibility should be popularised but not imposed. Corporate Governance." Vol. 8 (3), Pp. 330-341.

kutoa mchango kufanikisha miradi iliyoidhinishwa;[49] kukosa ushirikiano baadhi ya wakati; kutokufaidika wananchi wa maeneo husika, na kukosekana uaminifu na kuwepo ufisadi.[50]

# SURA YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA SERA NA MFUMO WA **KISHERIA**

## 3.1 Utangulizi

Sura hii ya Tatu inaelezea mtazamo wa Sera na Sheria mbali mbali ambazo kwa namna moja ama nyengine zinatoa muongozo juu ya masuala yanayohusiana na Uwajibikaji wa Wawekezaji kwa Jamii.

[49] Morsing, M and Schultz, M. (2006) "Corporate social responsibility communication: Stakeholder information, response and involvement strategies. Business Ethics:" A European Review. Vol. 15(4), Pp.323-338.

[50] Greening, D. W. and Turban, D. B. (2000) "Corporate social performance as a competitive advantage in attracting a quality workforce." Business and Society. Vol. 39, Pp. 254-280.

## 3.2 Miongozo mikuu

**Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984**

Katiba ni sheria muhimu inayozungumzia CSR kwa Zanzibar. Katiba ya Zanzibar, 1984 kama ilivyorekebishwa mara kwa mara, inaeleza kinga ya haki za lazima, wajibu na uhuru wa mtu binafsi. [51]

Katiba inaeleza kwamba kila mtu ana haki ya hifadhi ya maisha yake na haki ya kupata hifadhi kutoka kwa jamii kwa mujibu wa sheria.[52] Aidha Katiba Kifungu cha 17 inaeleza kwamba kinyume cha sheria kwa mtu yeyote kunyang'anywa mali yake isipokuwa masharti ya Katiba yawe yametimizwa ikiwemo kuchukuliwa ni kwa ajili ya ulinzi, usalama, mazingira, afya, maendeleo ya mji au mambo yanayoleta faida kwa wananchi kwa ujumla,[53] na kulipwa fidia inayolingana.[54]

Aidha Katiba inatoa haki na uhuru wa kushiriki katika shughuli za umma kwa mambo yanayowahusu,[55] kufanya kazi kwa masharti ya usawa wa kupata ujira kwa shughuli au kazi inayolingana.[56] Kifungu hiki kinakidhi matakwa ya Sheria za kazi ambazo zinahusishwa kwa kiasi kikubwa na uwajibikaji kwa jamii, na katika kujaribu kufanyia kazi masharti ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) (2008) na Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR) kuhusu mazingira ya kazi ya wafanyakazi na masuala ya haki za binadamu, Serikali ilitunga Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini za mwaka 2005.

---

[51] Sehemu ya Tatu ya Katiba
[52] Kifungu cha 13(1) ,na (2)
[53] Kifungu cha 17(a)
[54] Kifungu cha 17(c)
[55] Kifungu cha 21(1) na (2)
[56] Kifungu cha 21(4)

Kifungu cha 23 cha Katiba kinataka kila mtu kutii Katiba na sheria za nchi, kulinda maliasili, mali za nchi, na kuheshimu mali za mtu mwengine.[57] Suala la mali pamoja na kupiga vita aina zote za uharibifu na uhujumu wa uchumi pamoja na kulinda, kudumisha kuhifadhi mamlaka , ardhi, uhuru, na umoja.[58] Masuala ya ardhi katika eneo hili ni muhimu kutokana na athari yake kwa mashirika yanayomiliki sehemu kubwa ya ardhi kwa madhumuni ya uwekezaji, kuhakikisha wajibu wa kusaidia jamii hauongezi migogoro na jamii.

### (a) Dira ya maendeleo 2050[59]

Kupitia Dira ya Maendeleo inasisitiza kukuza msingi wa rasilimali watu wenye afya, ubunifu na tija, na kuunga mkono juu ya huduma za kijamii zinazotegemewa na ambazo zitaleta tija kwa watu wote ili kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya kitaifa na kimataifa.[60]

Miongoni mwa maeneo ambayo yamesisitizwa katika kuimarisha ustawi wa jamii ni yale maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa sana kwa wanajamii wenyewe kama vile masuala ya afya, elimu na ujuzi, masuala ya utafiti wa maeneo yenye uhitaji, huduma za maji, masuala ya utamaduni na michezo, masuala ya mazingira salama na ajira kwa wanajamii.

Hivyo kupitia Dira ya 2050, mamlaka zenye kusimamia maendeleo ya kijamii, ikiwemo wanajamii wenyewe, taasisi za Kiserikali, Asasi za Kiraia na hata

[57] Kifungu cha 23 (1) na (2)
[58] Kifungu cha 23(4)
[59] Zanzibar Development Vision 2050
[60] Pillar I

Makampuni ya Uwekezaji katika sekta tofauti kama vile utalii, mafuta na gesi, kilimo, uchumi wa buluu, viwanda na masoko zinatakiwa kutekeleza wajibu wao kwa jamii kuhakikisha kuwa wanajamii wanafaidika katika upatikanaji na uboreshaji wa yale maeneo muhimu kwa ajili ya ustawi wa jamii.[61]

**(b) Mkuza III**[62]

Mkuza umezungumzia ukuzaji uchumi na kupunguza umasikini, ambao unaitaka Serikali na taasisi zisizo za kiserikali katika kuchangia na kuweka mazingira mazuri ya ukuaji wa uchumi, kuendeleza uchumi na kuweka mazingira wezeshi kwa ukuaji wa kiuchumi huo, pamoja na kukuza usawa kwa watu masikini na wenye uwezo mkubwa.[63]

Aidha, MKUZA unahimiza upatikanaji wa huduma bora za kijamii ikiwemo elimu; afya; maji na usafi wa mazingira; makazi ya watu; upatikanaji wa chakula bora; usalama na ulinzi wa kijamii; na michezo na utamaduni.[64] MKUZA unaimarisha ulinzi wa kijamii na watendaji wasio wa Serikali ambao huchangia katika kupunguza umasikini, na pia kudhibiti athari za kimazingira kwa siku zijazo,[65] na kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora na mafunzo ya ujuzi ili kuongeza uwezo wa wanajamii kwa lengo la kuleta maendeleo ya taifa.[66]

**(c)Ilani ya CCM 2020-2025**[67]

[61] Pillar I, economic transformation of Zanzibar development vision 2050
[62] The Zanzibar strategy for growth and reduction of poverty III. (MKUZA III)
[63] Cluster 1.1.1
[64] Cluster 1.1.2
[65] Cluster 2.1.7 of the zanzibar strategy for growth and reduction of poverty III. (MKUZA III)
[66] Cluster 4.1.2 of the zanzibar strategy for growth and reduction of poverty III. (MKUZA III)
[67] Ilani ya chama cha mapinduzi 2020-2025

Ilani ya CCM ya 2020-2025 katika ibara ya 21 inatambua umuhimu wa sekta binafsi katika kuleta maendeleo kwa kuwa sekta hiyo ni moja ya nguzo muhimu za kujenga uchumi wa viwanda na maendeleo ya sekta nyenginezo za kiuchumi na kijamii kwa kushirkiana na Serikali katika uwekezaji.[68]

Aidha ibara ya 31 inasisitiza ongezeko la ajira kwa vijana na jamii kwa ujumla kutokana na kukua kwa uchumi katika sekta mbalimbali za uzalishaji na utoaji huduma pamoja na kutekeleza mikakati na mipango mbalimbali ikiwemo mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Kupitia Sura ya Tatu (3), Ilani inasistiza uimarishwaji na kuweka kipaumbele katika masuala ya maendeleo ya kijamii kama vile elimu, afya, maji na mazingira, pamoja na ustawi wa wazee.[69]

## 3.3 Sera

### (a) Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011[70]

Sera ya Utawala Bora imeainisha misingi ya utawala bora ikiwa ni pamoja na uwajibikaji na uwazi, utawala wa sheria na haki za binaadamu, kuzuia rushwa, ufanisi na tija, ushirikishwaji pamoja na kuzingatia matakwa ya wananchi. Katika suala la kuzingatia matakwa ya wananchi maana yake ni uwezo na utayari wa kushughulikia matakwa, maslahi na vipaumbele vya wananchi. Hii inamaanisha kuwa tayari kukubali mabadiliko ya kijamii, kutambua maslahi ya jumla ya wananchi na kuwa tayari kuangalia upya majukumu ya Serikali.[71] Aidha, kupitia sera hii ya utawala bora, moja ya malengo yake miongoni mwa

[68] Ibara ya 21, na 31 ya ilani ya CCM 2020-2025
[69] Sura ya (3) ya ilani ya CCM 2020-2025
[70] Sera ya utawala Bora ya mwaka 2011
[71] Sera ya utawala bora uk. 3, 4.

malengo mahasusi ni pamoja na kuhakikisha uheshimu wa majukumu ya kijamii kwa wawekezaji.[72]

### (b) Sera ya Uwekezajiiya mwaka 2005[73]

Malengo ya sera yamezingatia huduma za kijamii kwa wawekezaji.[74] Aidha, Sera inahakikupitia sera hii ya uwekezaji, katika mikakati ya sera ni kuhakikisha wawekezaji wanapatiwa haki zao za msingi zitakazowawezesha kufanya shughuli zao, na imewataka wawekezaji kutekeleza wajibu wao wa kulinda na kuheshimu haki za wadau na jamii kwa ujumla.[75]

### (c) Sera ya Mazingira ya mwaka 2013[76]

Sera hii inahakikisha ulindwaji na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika nyanja zote.[77]Aidha, Sera imesisitiza suala la uhifadhi wa mazingira katika sekta ya uwekezaji kama ni moja ya wajibu wa wawekezaji kuhakikisha kwamba wanafanya shughuli zao bila kukiuka Sheria na Kanuni za uhifadhi wa mazingira katika sekta ya utalii na uchimbaji n.k.[78]

### (d) Sera ya PPP ya mwaka 2014[79]

Sera hii imelenga kuhakikisha mashirikiano kati ya Serikali na taasisi binafsi na kwamba kampuni ambazo zinashirikiana na Serikali, zinatakiwa kutekeleza

[72] Sera ya utawala bora uk. 5
[73] Sera ya uwekezaji 2005
[74] Sera ya uwekezaji 2005 uk. 7
[75] Sera ya uwekezaji 2005 uk. 11
[76] The zanzibar environmental policy 2013
[77] Sera ya mazingira 2013 uk. 32
[78] Sera ya Mazingira 2013 uk. 13, 24
[79] Zanzibar Public Private Partnership Policy 2014

wajibu wao katika kuhifadhi na kulinda mazingira; kutoa huduma bora za kijamii pamoja na kulinda silka na tamaduni za Wazanzibari.[80]

Aidha, kupitia Sera hii, mashirikiano ya Serikali na taasisi binafsi, yamewekewa maeneo muhimu ya kuzingatia kama ni miongozo ya utekelezaji wa ushirika na Sera inahhakikisha kwamba Kampuni ambazo zinaingia katika makubaliano ya ubia na Serikali, yana uwezo wa kujitosheleza katika kutekeleza wajibu wao kwa jamii.[81]

### (e) Sera ya Utalii ya mwaka 2017[82]

Mazingira ni sekta muhimu kwa utalii, Sera inaelekeza mamlaka ya mazingira kuhakikisha kwamba eneo linalotaka kutumika katika uwekezaji haliathiri mazingira, na imetaka kufanywa kwa tathmini ya mazingira (EIA).[83] Sera inataka kusifanywe ujenzi hadi EIA ipatikane na majibu ya utafiti wa EIA kwa kuwasilishwa "Environmental Statement".

Sera inahakikisha kunalindwa mazingira katika sekta hii ni muhimu, madhara ya mazingira, haki za watu, matumizi ya fukwe na bahari, na kulinda mazingira ya bahari matumbawe, uvuvi na mazingira ya pwani yanawanufaisha wananchi.

[80] Ibid uk. 6
[81] Ibid UK. 18
[82] Sera ya Utalii ya mwaka 2017
[83] Environmental Impact Assessment

### (f) Sera ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2016

Malengo makuu ya Sera ni kutoa nafasi kwa wawekezaji katika sekta hiyo, kwa kukuza uchumi wa nchi, na kuimarisha maendeleo ya Wazanzibari hususani katika kupunguza umasikini, kuimarisha afya na usalama pamoja na kujenga mazingira bora na endelevu.[84] Aidha Sera inataka sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kutatua mahitaji ya wanajamii pamoja na ulinzi wa mazingira yao kwani kufanikiwa katika sekta hii ya mafuta na gesi ni kwa ajili ya maendeleo ya Wazanzibari.

## 3.4 Sheria

### (a) Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar Nam. 14 ya mwaka 2018

Sheria hii imeelezea wajibu na makatazo kwa wawekezaji kwa kuwashurutisha wawekezaji kuendesha biashara zao kwa mujibu wa mpango wa biashara ambao umepitishwa na Mamlaka pamoja na kuitii Sheria hiyo, Sheria za mazingira na Sheria nyengine za Zanzibar[85] Wawekezaji wamekatazwa kuendesha shughuli kinyume na Sheria au kanuni zozote zinazotumika Zanzibar.

### (b) Sheria ya Mafuta na Gesi Zanzibar Nam. 6 ya mwaka 2016

Sheria imeweka utaratibu kwa wawekezaji wanaokuja kuwekeza katika sekta ya mafuta na gesi Zanzibar kutekeleza wajibu wao kwa jamii. Kupitia kifungu cha 137 kimewataka wawekezaji pamoja na wakandarasi kuandaa mpango wa

[84] Chapter 4: Policy Framework. UK 49
[85] Kifungu cha 21(b), (o) 22(g)

uwajibikaji kwa Jamii kwa mwaka kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa kwa kuzingatia mpango mkakati wa uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii Zanzibar kwa upande wa mazingira, uchumi, jamii na tamaduni.[86]

### (c) Sheria ya Utalii Zanzibar Nam. 6 ya mwaka 2009

Sheria hii katika kifungu cha 27 imezungumzia kwa kina suala la uwajibikaji kwa jamii kupitia taasisi za uwekezaji katika sekta ya utalii,[87] na kumtaka kila msimamizi na mmiliki wa biashara ya utalii iliyosajiliwa kuandaa sera na mkakati wake maalum wa utekelezaji wa majukumu yao kwa jamii hususani katika suala la kutoa uwelewa juu ya kudhibiti na kupiga vita maambukizi ya HIV pamoja na madawa ya kulevya nchini, lakini pia kuheshimu tamaduni za wazanzibari pamoja na kutunza mazingira, kubwa zaidi ni kushiriki katika kuchangia kwa namna tofauti katika kuimarisha ustawi wa jamii katika sehemu husika.[88]

### (d) Sheria ya Kampuni Zanzibar Nam. 15 ya mwaka 2013

Sheria ya Kampuni haikuainisha vifungu vya wazi vya CSR lakini imeweka baadhi ya vifungu ambavyo vimezingatia misingi ya wajibu wa kusaidia jamii. Sheria inataka kampuni kufanyakazi kwa kuzingatia malengo yake na kuinua uchumi[89] na kutanua wigo au kubadilisha sehemu ya jamii au shughuli za jamii.[90]

---

[86] Kifungu cha 137
[87] Kifungu cha 27
[88] Kifungu cha 27
[89] Kifungu cha 7(1)(a)
[90] (kifungu cha 7(1)(c)

Aidha Kampuni inatakiwa ifanye kazi zake kwa uamimifu na nia njema katika utekelezaji wa majukumu yake,91 na Mkurugenzi anatakiwa kufanya kazi zake kwa uangalifu, utaalam na ujuzi Pamoja na kutumia utaalam mwengine ambao Mkurugenzi anatakiwa atumie,92 kwa lengo la kutimiza maslahi ya kampuni , wananchi, wadau na taifa kwa ujumla.

**(e) Sheria ya Mamlaka ya Bahari ya Nam. 3 ya mwaka 2009[93]**

Mamlaka ya Bahari ni miongoni mwa taasisi wadau kwa suala zima la mazingira visiwani humu. Hivyo miongoni mwa kazi zinazofanywa na Mamlaka hiyo ni kuhakikisha tafiti zote za kimazingira (Environmental Impact Assement and Strategic Environment Project Analysis) zinafanyika kwa miradi yote ambayo itaonekana kuwa na madhara ama kuleta matokeo chanya kwa upande wa sekta za biashara na uwekezaji. Tathmini hizi zinatakiwa zifanyike kwa ushirikiano wa Taasisi zilizo na wajibu wa kutunza mazingira.[94]

Kwa madhumuni ya kudhibiti na kulinda uharibifu wa mazingira ya bahari, Sheria imeeleza kwamba kwa yeyote ambaye atafanya kinyume chake atatozwa faini inayoendana na madhara ya mazingira ya bahari aliyoyasababisha.

**(f) Sheria ya PPP Nam. 8 ya mwaka 2015**

Sheria hii, inawahakikishia mashirika binafsi kuwa na haki ya kufaidika bila ya kikomo na zile stahiki na haki zote walizokubaliana kwa mujibu wa makubaliano ya ushirika baina ya Serikali na mashirika binafsi. Aidha

[91] Kifungu cha 185
[92] Kifungu cha 188
[93] Sheria ya mamlaka ya bahari Zanzibar nam. 3 ya mwaka 2009
[94] Sec.5 (1) (t) Sheria ya Mamlaka ya Baharini namba 3/2009

mashirika ama wawekezaji nao watakuwa na wajibu wa kutekeleza masharti yote waliyokubaliana kuyatekeza kwa mujibu wa sheria.[95] Sheria inaipa nafasi Serikali miongoni mwa masharti watakayoweka dhidi ya sekta binafsi ni pamoja na kuweka wajibu kwa jamii juu ya kuimarisha ustawi wa jamii husika.

**(g) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Nam. 3 ya mwaka 2015**[96]

Sehemu ya pili ya Sheria hii imeweka vifungu ambavyo vimeweka wajibu kwa kila mtu kulinda na kuhifadhi mazingira kwa ustawi wa jamii na vivazi vya baadae.[97]

Aidha, katika Sheria hii imeainisha pia haki za msingi ambazo pia ni haki ya kikatiba ya kila mtu kuishi katika mazingira safi na salama.[98] Sehemu ya Kumi na Moja ya Sheria hii imeweka kifungu cha makatazo ya uchafuzi wa mazingira kwa kuzingatia Sheria yoyote inayosimamia mazingira Zanzibar.[99]

**(h) Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma Nam. 6 ya mwaka 2021**

Sheria imeweka vifungu mbalimbali vinavyosimamia masuala ya uwajibikaji kwa jamii kupitia wawekezaji. Aidha Sheria imefafanua mipaka ya matumizi katika Sheria ikiwemo taasisi za uwekezaji za umma, taasisi za umma kwa upande wa usimamizi wa mali pamoja na taasisi yoyote ya umma itakayotajwa na Waziri.[100]

[95] Kifungu cha 17
[96] The Zanzibar Environmental Management Act 3, 2015
[97] Kifungu cha 3
[98] Kifungu cha 4
[99] Kifungu cha 51
[100] Kifungu cha 2, Sheria ya Ofisi ya Msajili wa hazina na usimamizi wa mali za Umma Nam. 6 ya mwaka 2021

Kupitia kifungu cha 6(d), sheria inazungumzia moja miongoni mwa majukumu ya ofisi ni kukuza maadili ya utawala bora katika miamala yote ya biashara ikijumuisha utoaji wa miongozo kwa taasisi za uwekezaji za umma kwenye mambo yanayohusiana na bajeti, mipango mkakati, mipango ya kibiashara, mipango ya uwekezaji na mambo mengine yote yanayohusiana na hayo katika kutekeleza sera za serikali kwenye taasisi za uwekezaji za umma[101] Aidha, kifungu cha 9(b) kinazungumzia moja miongoni mwa majukumu ya Msajili wa Hazina ni pamoja na kuidhinisha mgao wa faida wa mwaka na kutangaza mgao, ziada au, mchango wa taasisi za uwekezaji za umma.

Vile vile, sheria hii imeweka majukumu kwa wakurugenzi wa taasisi katika wajibu wa wawekezaji kwa jamii ikiwemo kusimamia maadili, uweledi, pamoja na hadhi ya watendaji wa taasisi ya uwekezaji ya umma, lakini pia itasimamia matumizi ya miradi ya maendeleo.[102]

Sheria inaanzisha mpango mkakati pamoja na mkataba wa utendaji kupitia sehemu ya 4 ya sheria hii inayozungumizia juu ya uwajibikaji wa taasisi za uwekezaji za umma ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango mkakati kwa mujibu wa miongozo itakayotolewa na Msajili wa Hazina.[103] Ili kuhakikisha majukumu haya yanasimamiwa vyema, sheria inawataka watendaji wakuu wa taasisi kungia mkataba na Bodi ya Wakurugenzi kwa mujibu wa vigezo na masharti yalioainishwa na Msajili wa Hazina.[104]

[101] Kifungu cha 6(d)
[102] kifungu cha 26(d),(k)
[103] kifungu cha 32
[104] Sheria ya Ofisi ya Msajili wa hazina na usimamizi wa mali za Umma nambari 6 ya mwaka 2021. Sehemu ya 4 ya sheria, Kifungu cha 32,33.

### (i) Sheria ya Mamlaka ya Tawala za Mikoa Nam. 8 ya mwaka 2014

Sheria hii imeweka baadhi ya vifungu vyenye mnasaba na suala zima la uwajibikaji kwa jamii kupitia vifungu vya 12, 14, na 18 ambavyo kwa pamoja vinazungumzia majukumu ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya pamoja na Sheha wa shehia husika katika kusimamia na kuhakikisha utekelezaji wa Sera, Sheria mipango na miongozo ya Serikali. Vifungu vimeweka pia majukumu ya kudumisha ulinzi na usalama katika nyanja zote, kuhakikisha utii wa haki za binaadamu pamoja na kuongoza na kusimamia programu pamoja na harakati zote za kimaendeleo ndani ya Mkoa, Wilaya au Shehia.

# SURA YA NNE

## 4.0 UTANGULIZI

Sura hii inaainisha maoni, ushauri na mapendekezo ya wadau mbali mbali yaliyotolewa wakati wa vikao vilivyoandaliwa kwa madhumuni ya kukusanya taarifa kuhusiana na utafiti wa eneo la uanzishwaji wa utaratibu wa Kisheria kuhusiana na Wajibu wa Wawekezaji kwa Jamii. Msingi wa Tume kukusanya maoni kwa wadau unatokana na kifungu cha 10 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya Mwaka 1986 kinachoitaka Tume kukusanya maoni ya wadau wengi kwa kadri inavyowezekana wakati waufanyaji tafiti au mapitio ya Sheria. Tume imeyagawa maoni hayo katika makundi mawili ambayo ni kundi la maoni ya Kisheria na kundi la maoni ya Kiutendaji kama inavyoainishwa hapo chini.

## 4.1 Makundi ya Wadau Walioshiriki na Taasisi Walizotoka

Jumla ya taasisi Ishirini na Moja (21) za Serikali na Binafsi zilishirikishwa katika upatikanaji wa ushauri, mapendekezo na maoni kuhusu upatikanaji wa utaratibu wa kisheria utakaotumika katika uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii kwa maeneo uwekwzaji ulipofanyika.

## 4.2 Maoni ya Wadau

Maoni ya wadau yamegawika katika sehemu kuu mbili ambazo ni maoni ya kisheria na maoni ya kiutendaji kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Maoni ya Kisheria

#### (a) Kuanzishwa kwa Sera maalum

Wadau wamependekeza kuwepo na Sera maalum ambayo itatoa mwongozo wa kutosha juu ya suala la uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii kabla ya kuja na sheria husika ili kuweza kupata sheria iliyo bora zaidi. Sera ianishe maeneo ya kuzingatiwa, upeo wa CSR, na wajibu wa Serikali katika utekelezaji wa miradi ya CSR.

Imependekezwa Sera iainishe misingi ya kutoa huduma za kijamii kwa kuzingatia biashara ya taasisi au mwekezaji, kiwango cha mtaji, uwezo wa kiwango cha kuingiza faida n.k ambapo sifa hizo zitazingatiwa katika uwajibikaji wa utoaji wa huduma za wanajamii husika katika kuimarisha ustawi wa jamii hizo ikiwa ni moja ya miongoni mwa aina za uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii.

#### (b) Kuanzishwa kwa Sheria

Wadau wamependekeza kuanzishwa Sheria ambayo itaweka masharti ya msingi na kusimamia masuala ya Uwajibikaji kwa Jamii. Hatua hii itafanya kuwa na mwongozo maalum ambao sheria mbali mbali na mamlaka za usimamizi kufuata masharti ya sheria hiyo wakati wa kusimamia maeneo yaliyo chini ya CSR. Aidha sheria itaainisha jukumu la wawekezaji, kampuni za ndani, mashirika ya umma na taasisi nyengine katika eneo la uwajibikaji kwa jamii.

### (c) Uwepo maeneo maalum ya uwajibikaji kwa jamii

Wadau wamependekeza uwepo wa maeneo maalum ambayo yatahusishwa na uwajibikaji kwa jamii, na imependekezwa maeneo ya kuzingatiwa yajumuishe misaada; masuala ya kisayansi; maendeleo ya vijana na michezo; masuala ya kitamaduni au elimu; huduma kwa wastaafu na wazee; ustawi wa jamii; uendelevu wa mazingira; afya; na msaada na usaidizi wakati wa maafa.

### (d) Adhabu kwa wawekezaji wasiowajibika

Wadau wamependekeza kuwekwa adhabu kwa wawekezaji na mashirikika au taasisi zitakazotakiwa kutekeleza uwajibikaji kwa jamii, ili kuzifanya zitekeleze majukumu yao kwa kuzingatia Katiba na misingi ya utawala bora. Aidha taasisi na wawekezaji watakiwe kufuata misingi ya miongozo ya kibiashara kama ni njia moja wapo ya kujenga uimara katika kukuza na kuendesha biashara zao na kufuata Sheria za Nchi.

### (e) Mpango wa CSR

Wadau wamependekeza kampuni, wawekezaji na taasisi husika zitakiwe kuweka mpango maalum wa kutekeleza maeneo ya CSR, na mpango huo uwasilishwe pamoja na ripoti chini ya sheria ya kampuni, sheria ya Msajili wa Hazina na sheria nyengine zinazosimamia taasisi hizo.

### (f) Mfuko wa mradi wa Wajibu wa Wawekezaji.

Ili kuhakikisha shughuli za CSR zinakuwa endelevu na zinasaidia wananchi, imependekezwa wawekezaji na taasisi husika zitakiwe kutenga kima maalum cha fedha au asilimia fulani kutoka katika bajeti zao za kila mwaka kwa ajili ya shughuli za kuwajibika kwa jamii.

### (g) Usimamizi wa miradi na eneo la CSR

Wadau wamependekeza kuwekwa taasisi maalum ambayo itaratibu shughuli za uwajibikaji kwa jamii na kutoa taarifa Serikalini juu ya taasisi na wawekezaji ambao wameshiriki katika uwajibikaji kwa jamii. Aidha taasisi hiyo ipewe kazi ya kufanya tathmini ya miradi na maeneo yanayochangiwa na wawekezaji au taasisi na kushauri iwapo kumetolewa huduma stahili, au ukubwa wa athari katika ameneo ya uwekezaji zimeweza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa. Taasisi hii ipime matokeo ya msaada au shughuli za CSR na usimamizi wake kwa upande wa Serikali.

### (h) Eneo linalotakiwa kufaidika na miradi ya CSR

Wadau wamependekeza kuwekwa miongozo ambayo itafanya jamii ambayo wawekezaji wanafanya shughuli zao inafaidika kwa kiasi fulani na dhana ya uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii. Hata hivyo utaratibu huo usimfunge mwekezaji au taasisi kuhudumia eneo ambalo anaona lina mahitaji makubwa zaidi.

### (i) Elimu kwa wananchi

Imependekezwa wananchi wapewe elimu kuhusu uwajibikaji kwa jamii, pamoja na taasisi za Serikali ikiwemo Halmashauri na Mabaraza ya Miji ili kuweza kutoa ushauri na kupendekeza maeneo ambayo yatasaidia zaidi wananchi. Aidha elimu itolewe kwa taasisi binafsi, wawekezaji, kampuni na wadau wengine wanaohusika na CSR.

### (j) Ushirikiano baina ya taasisi

Katika kutekeleza uwajibikaji kwa jamii, wadau wamependekeza kuwepo ushirikiano mzuri baina ya taasisi na mamlaka zote ambazo zitakuwa na wajibu kwa namna moja ama nyengine katika masuala ya uwekezaji tokea ngazi za chini hadi Taifa.

## SURA YA TANO

## 5.0 MIKATABA YA KIMATAIFA NA UZOEFU WA NCHI MBALIMBALI

### 5.1 Utangulizi

Uhusiano wa CSR na mikataba ya kimataifa jambo la hivi karibuni, majaribio ya kwanza ya kuzingatia eneo la CSR kimataifa yalionekana na Umoja wa Mataifa katika miaka ya 1950,[105] lakini rejea kuhusu eneo hili zilianza miaka ya 1920, kama matokeo ya mjadala juu ya hitaji la wasimamizi wa kampuni kutozingatia maslahi ya wanahisa pekee bali pia maslahi ya wadau wengine.[106]

Katika miaka ya 1960 na 1970, kuongezeka kwa umuhimu wa biashara za kimataifa na kuongezeka kwa nguvu na ushawishi katika masuala ya ndani kulizua maswali kuhusu utawala wa kampuni za kimataifa. Umoja wa Mataifa (UN) ulijaribu kushughulikia suala hili katika ngazi ya kimataifa kupitia Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) na Shirika la Kazi Duniani

[105] John Ruggie Protect, Respect and Remedy: A Framework for Business and Human Rights UN Doc. A/HRC/8/5 7 April 2008

[106] Braithwaite, J. (2006). Responsible Regulation and Developing Economies', World Development, 34(5): 884-898.

(ILO), ambayo yalipitisha mambo mawili muhimu katika eneo hili. Miongozo iliyopitishwa ni pamoja na Miongozo ya OECD kwa Biashara za Kimataifa (OECD Miongozo), iliyopitishwa mwaka 1976[107] na Azimio la Utatu la Kanuni za ILO kuhusu Biashara za Kimataifa na Sera ya Kijamii (Tamko la MNE) lililopitishwa mnamo 1977.[108]

Vyombo vya CSR vya kimataifa vyenye ushawishi mkubwa zaidi ni Miongozo ya OECD, Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa, na Azimio la ILO la 1998. Miongozo ya OECD ni mapendekezo yanayotakiwa kushughulikiwa na Serikali kwa MNEs. [109] Ingawa hazifungi kisheria kuhusu MNEs, Mataifa ya OECD yamekubali kuzingatia Miongozo na kuhimiza kampuni zao kuzingatia popote yatakapokuwa yanafanya kazi.[110]

## 5.2 Umoja wa Mataifa –UN

Miongozo ya Umoja wa Mataifa ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1976 na imetoa mapendekezo kuhusu haki za binadamu, ajira na mahusiano ya viwanda, mazingira, masuala ya rushwa, maslahi ya watumiaji, sayansi na teknolojia, ushindani, na kodi.[111] Aidha Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa ulizinduliwa Septemba 2000 na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa,

---

[107] the OECD Guidelines for Multinational Enterprises (OECD Guidelines), adopted in 1976

[108] the ILO Tripartite Declaration of Principles concerning Multinational Enterprises and Social Policy (MNE Declaration) adopted in 1977

[109] Kathryn Gordon, The OECD Guidelines and Other Corporate Responsibility Instruments: A Comparison, in OECD GUIDELINES FOR MULTINATIONAL ENTERPRISES: ANNUAL REPORT 2001 (OECD, Working Paper No. 2001/15, 2001) available at http://www.oecd.org/dataoecd/46/36/2075173.pdf.

[110] Braithwaite, J. (2006). 'Responsible Regulation and Developing Economies', World Development, 34(5): 884-898.

[111] United Nations. (2011). Guiding Principles on Business and Human Rights. Implementing the 'Protect, Respect and Remedy Framework'. New York and Geneva: United Nations.

ambaye alitoa wito kwa viongozi wa biashara duniani kutunga sheria katika uhusiano wa biashara.[112]

Kanuni na Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Kibinadamu ina nafasi muhimu zaidi ikiwemo kanuni za Maadili za Umma.[113] Kanuni hizo zimezingatia haki za binadamu na mashirika ya kimataifa na mashirika mengine ya biashara, wajibu wa Kampuni na mashirika kuheshimu haki za binadamu na upatikanaji wa suluhu.[114] Kanuni pia ziliidhinishwa kwa kauli moja na Baraza la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa tarehe 16 Juni 2011, na kuifanya kuwa kanuni ya kwanza ya Maadili ya Umma kuhusu biashara na haki za binadamu iliyoidhinishwa na Umoja wa Mataifa.[115]

Aidha Kanuni zimekusudiwa kutekelezwa na nchi na kampuni, ambapo Umoja wa Ulaya tayari umezikaribisha nchi wanachama kuandaa mipango ya utekelezaji ya kitaifa na nchi kadhaa za Ulaya, zimewasilisha mipango hiyo ya utekelezaji.[116]

Kanuni nyengine muhimu katika Uwajibikaji na maadili kwa umma zinajumuisha matamko husika ya ILO, yaani Azimio la Utatu (Tripartite) la

[112] Transnational Investments and Operations on the Lands of Indigenous Peoples, U.N. ESCOR, Agenda Item 15, at 4, U.N. Doc. E/CN.4/Sub.2/1994/40 (1994).
[113] Guiding Principles on Business and Human Rights: Implementing the United Nations "Protect, Respect and Remedy" Framework of the UN of 2011, available online at https://www.ohchr.org/Documents/Publications/GuidingPrinciples BusinessHR_EN.pdf

[114] John Ruggie, Guiding Principles on Business and Human Rights: Implementing the United Nations "Protect, Respect and Remedy" Framework, report of 21 March 2011, A/HRC/17/31 (2011).
[115] Resolution A/HRC/RES/17/4 of the UN Human Rights Council of 16 June 2011.
[116] European Commission (fn. 7), at 14; Swiss Federal Council, Bericht über die Schweizer Strategie zur Umsetzung der UNOLeitprinzipien für Wirtschaft und Menschenrechte, report of 9 December 2016, available online at https:// www.newsd.admin.ch/newsd/message/attachments/46597.pdf

ILO.[117] Tamko la Kanuni zinazohusu Biashara za Kimataifa na Sera ya Kijamii, ambazo pia zinarejelea Azimio la Kanuni na Haki za Msingi katika Kazi.[118]

Kwa kulinganisha, Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa una seti maalum zaidi ya viwango. Kanuni Kumi ambazo Mkataba wa Kimataifa ulianzishwa zinahusu maeneo haki za binadamu, kazi, mazingira na kupambana na rushwa.[119]

## 5.3 OECD

OECD ni chombo muhimu kinachoshughulikia Miongozo na Kanuni za Uwajibikaji wa Biashara Ulimwenguni, kwa Biashara za Kimataifa.[120] Mkataba wa Kimataifa na Global Sullivan Principles huweka wazi kanuni za kitabia, na kutoa maelezo ya kina mapendekezo kwa kampuni.[121] Miongozo ya OECD, ina mapendekezo ya hiari kuhusu haki za binadamu, ajira, mahusiano ya viwanda, mazingira, masuala ya rushwa na maslahi ya watumiaji, ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1976.[122]

Aidha miongozo hiyo ni mapendekezo ya serikali kwa makampuni za kimataifa (MNEs) zinazofanya kazi ndani au kutoka nchi mbalimbali. Miongozo husaidia

[117] ILO (2016) Proposed modalities to review the Tripartite Declaration of Principles concerning Multinational Enterprises and Social Policy, GB.326/POL/8.

[118] Tripartite Declaration of Principles concerning Multinational Enterprises and Social Policy of the ILO of 2017, available online at https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---ed_emp/---emp_ent/---multi/documents/publication/wcms_094386.pdf 17 See the database on the website of the UN Global Compact, available online at https://www.unglobalcompact.org/what-isgc/participants

[119] United Nations. (2011). Guiding Principles on Business and Human Rights. Implementing the 'Protect, Respect and Remedy Framework'. New York and Geneva: United Nations.

[120] OECD Guidelines for Multinational Enterprises of the OECD of 2011, available online at http://www.oecd.org/daf/inv/ mne/48004323.pdf

[121] Gordon, K. (2001), "The OECD Guidelines and Other Corporate Responsibility Instruments: A Comparison", OECD Working Papers on International Investment, 2001/05, OECD Publishing. http://dx.doi.org/10.1787/302255465771

[122] Gordon, K. ibid

kuhakikisha kwamba MNEs zinaafanya kazi na kwa matarajio ya jamii katika masuala mbalimbali na kuzingatia maadili ya biashara.[123]

Msingi wa Miongozo ya OECD katika uwajibikaji wa jamii unasaidia kujenga mazingira ya kujiamini na kutabirika kati ya biashara, wafanyakazi, Serikali na jamii kwa ujumla.[124] Miongozo ya OECD inataja utawala bora wa kampuni au shirika kama sera ya jumla itakayokuwa kuheshimiwa, na inaambatana na njia za ufuatiliaji.[125]

OECD ina malengo ya Mpango wa wafadhili wa Kuripoti (GRI) na Uwajibikaji kwa Jamii,[126] yanalenga kusaidia Kampuni kwenda kujitolea zaidi kwa kuzingatia mipango ya uwajibikaji wa Kampuni au shirika katika ufuatiliaji na utoaji taarifa, kwa kutoa viwango vya kimataifa.[127]

---

[123] Kathryn Gordon (2001) The OECD Guidelines and Other Corporate Responsibility Instruments: A COMPARISON, This paper forms part of an OECD publication entitled OECD Guidelines for Multinational Enterprises: Annual Report 2001 which was published in December 2001. WORKING PAPERS ON INTERNATIONAL INVESTMENT Number 2001/5

[124] OECD Guidelines for Multinational Enterprises: (revised in 2000) The Guidelines are recommendations covering nine areas of business conduct addressed by governments to multinational enterprises. While observance of the recommendations by enterprises is purely voluntary, adhering governments sign a binding decision to participate in Guidelines implementation and to promote their observance by enterprises operating in or from their territory.

[125] OECD Principles of Corporate Governance (Paris, OECD, 2004) available at http://www.oecd.org/dataoecd/32/18/31557724.pdf For this position see Paddy Ireland and Renginee Pillay "Corporate Social Responsibility and the New Constitutionalism" in Peter Utting (ed). Corporate Social Responibility and Regulatory Governance: Towards Inclusive Development? (UNRISD/PalgraveMacmillan forthcoming) available at http://kar.kent.ac.uk/11696/

[126] 8000 (SA 8000)

[127] The objectives of the sponsors of the Global Reporting Initiative (GRI) and Social Accountability 8000 (SA 8000) are quite different than those of the other five instruments. Both seek to help companies go beyond the "commitment phase" of corporate responsibility initiatives into the monitoring and reporting phases. By providing international standards for external verification of management practices and for non-financial performance reporting, SA 8000 and the GRI hope to enhance the credibility of individual company initiatives.

## 5.4 Shirika la Kazi Duniani

Shirika la Kazi Duniani ni wakala maalum wa Umoja wa Mataifa, ambao inalenga kukuza haki ya kijamii na haki za binadamu na kazi zinazotambulika kimataifa. Shirika hili lilianzishwa mwaka 1919 likiwa na mikakati minne inayohusu; kukuza na kutambua viwango na kanuni za kimsingi na haki kazini; kutengeneza fursa kubwa zaidi kwa wanawake na wanaume kupata ajira zenye staha na mapato; Kuimarisha ulinzi na ufanisi wa ulinzi wa kijamii kwa wote; na kuimarisha utatu na mazungumzo ya kijamii.[128] Shughuli nyengine zinazofanywa na ILO ni pamoja na kuendeleza sera na programu za kimataifa za kukuza haki za msingi za binadamu, kuboresha mazingira ya kazi na maisha, na kuongeza fursa za ajira.[129]

Katika mikutano mingi, ILO inaeleza kuwa mjadala kuhusu haki za binadamu, kama sehemu ya uwajibikaji wa kijamii wa Kampuni au taasisi, na zinapaswa kuzingatia misingi iliyoainishwa katika Azimio la Utatu la Kanuni zinazohusu Biashara za Kimataifa na Kijamii.[130]

Tamko la Utatu la ILO, lina kanuni za kimsingi katika nyanja za ajira, mafunzo, mazingira ya kazi na mahusiano ya viwanda, ilichapishwa kwa mara ya kwanza

[128] Among the ILO Conventions, eight have been identified as fundamental, in that they cover subjects that are considered as fundamental principles and rights at work.

(a) Freedom of Association and Protection of the Right to Organise Convention (No. 87), 1948
(b) Right to Organise and Collective Bargaining Convention (No. 98), 1949
(c) Forced Labour Convention (No. 29), 1930
(d) Abolition of Forced Labour Convention (No. 105), 1957
(e) Minimum Age Convention (No. 138), 1973
(f) Worst Forms of Child Labour Convention (No. 182), 1999
(g) Equal Remuneration Convention (No. 100), 1951
(h) Discrimination (Employment and Occupation) Convention (No. 111), 1958

[129] ibid

[130] Tripartite Declaration of Principles Concerning Multinational Enterprises (MNE) and Social Policy

mwaka 1978 na zaidi kurekebishwa mwaka 2017.[131] Azimio la Utatu la ILO linakusudiwa kuwa lisilofunga na kimsingi halina utaratibu rasmi wa utekelezaji wa masharti yake.[132] Kwa njia hii lengo la ICSR la uzingatiaji wa haki za wafanyakazi linapewa nguvu halisi kupitia sheria za utawala bora.[133]

Zaidi ya hayo, muundo wa kipekee wa utatu wa ILO na juhudi zake za kukuza mazungumzo ya kijamii ni muhimu katika kuwezesha ushiriki wa wadau wote katika CSR. Kwa kuwa inasaidia kukuza mazungumzo kati ya Serikali, mashirika ya wafanyakazi na waajiri na kwa kutoa msaada na kuelewa vyema mwelekeo wa kazi wa CSR.

### 5.4.1 Azimio la Kanuni na Haki za Msingi Kazini

Mnamo 1998, Mkutano wa Kimataifa wa Kazi ulipitisha Azimio la Msingi Kanuni na Haki Kazini (Tamko la Msingi), lililotokana na Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Jamii mwaka 1995 uliofanyika Copenhagen. Azimio lilizingatia haki za msingi za wafanyakazi, uhuru wa kujumuika, haki ya kupanga na kujadiliana kwa pamoja, malipo sawa kwa kazi ya thamani sawa, na kuondoa ubaguzi katika ajira.[134]

---

[131] The Universal Declaration of Human Rights; The International Labour Organization's Declaration on Fundamental Principles and Rights at Work; The Rio Declaration on Environment and Development and The United Nations Convention Against Corruption.

[132] (2014). Implementation strategy for the follow-up mechanism of and promotional activities of the Tripartite Declaration of Principles concerning Multinational Enterprises and Social Policy (MNE Declaration), GB.320/POL/10

[133] European rules on worker participation in MNEs 9 See further Report of the Special Representative of the Secretary-General on the issue of human rights and transnational corporations and other business enterprises Human rights impact assessments - resolving key methodological questions (UN Doc A/HRC/4/74, 5 February 2007)

[134] Declaration on Fundamental Principles and Rights at Work In 1998 the International Labour Conference adopted the Declaration on Fundamental Principles and Rights at Work (Fundamental Declaration). Its origins are to be found at the UN World Summit for Social Development in 1995 held in Copenhagen

ILO inahimiza hasa nchi zinazoendelea na biashara ndani yake kutumia Dawati la Usaidizi la ILO,[135] hata hivyo vyombo vya ILO katika vifungu vya CSR vinahitaji kufanyiwa kazi zaidi ili vilenge kuimarisha mifumo ya udhibiti wa kitaifa katika nchi za nyumbani na mwenyeji.

Kwa kuongezeka hata hivyo, ILO imehusika moja kwa moja katika ngazi ya biashara binafsi, yaani kupitia utoaji wa miongozo (k.m. Tamko la MNE), kwa kusaidia biashara katika kukuza viwango vya kimataifa vya kazi. [136] Azimio la MNE la ILO linachunguza masuala ya CSR na vipimo vifuatavyo vinazingatiwa ikiwemo maendeleo ya mpango huo katika biashara na uwekezaji; ushiriki wa ILO katika ngazi ya kampuni; viwango tofauti vya uhalalishaji; na kutilia mkazo ushirikishwaji wa wadau mbalimbali.[137]

### 5.4.2 Azimio la MNE

Azimio la MNE ndicho chombo pekee cha ILO ambacho kina mapendekezo ya kampuni ya biashara pamoja na Serikali na mashirika ya waajiri na wafanyakazi.[138] Lengo la Azimio la MNE ni kuhimiza mchango chanya ambao kampuni na mashirika ya kimataifa yanaweza kuleta maendeleo ya kiuchumi

[135] EESC, 2015
[136] See ILO (2016) for the proposed modalities to review the MNE Declaration.
[137] ILO: (2014). Implementation strategy for the follow-up mechanism of and promotional activities of the Tripartite Declaration of Principles concerning Multinational Enterprises and Social Policy (MNE Declaration), GB.320/POL/10.
[138] ILO, 2017: The ILO Tripartite Declaration of Principles Concerning Multinational Enterprises and Social Policy (MNE Declaration) was negotiated and adopted by governments, employers and workers in 1977- Geneva:, https://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---ed_dialogue/---actrav/documents/publication/wcms_627351.pdf

na kijamii na kupunguza na kutatua matatizo ambayo shughuli zao mbalimbali zinaweza kusababisha.[139]

Azimio linatoa miongozo ya jinsi kampuni inavyopaswa kutumia kanuni zinazotokana na viwango vya kimataifa vya kazi vinavyohusu ajira, mafunzo, hali ya kazi na maisha, na mahusiano ya viwanda. Azimio linaanza na sehemu ya sera za jumla ambayo ina mapendekezo ya kufikia maendeleo endelevu na kuheshimu haki za binadamu mahali pa kazi, kuheshimu viwango vya kimataifa kuhusu haki za binadamu na kazi; na heshima kwa mujibu wa sheria za kitaifa na wajibu wa kimataifa unaokubalika. [140]

Kuhusu ajira, kanuni za Tamko la MNE linahakikisha uendelezaji wa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, usawa wa fursa na matibabu, na usalama wa ajira.[141] Katika mahusiano, ya viwanda, Azimio la MNE linahimiza mashirika ya kimataifa kuzingatia viwango visivyofaa zaidi, uhuru wa kujumuika na haki ya kujipanga, na Mashirika ya kimataifa pia yanahimizwa kusaidia katika maendeleo ya makubaliano ya pamoja yenye ufanisi.[142]
Hata hivyo, utekelezaji wa jukumu la ILO kuhusiana na vifungu vya CSR katika mikataba inapaswa kutekelezwa. Kwa mfano, kwa upande wa EU, Kamati ya Uchumi na Kijamii ya Ulaya kuhusu CSR inataka kujumuishwa katika mikataba ya biashara ya vyombo vya CSR vinavyotambuliwa kimataifa ikiwa ni pamoja na marejeo ya ILO.[143]

---

[139] OECD Guidelines for Multinational Enterprises, 27 June 2000, p.14. http://www.oecd.org/dataoecd/56/36/1922428.pdf
[140] paragraphs 8-12
[141] paragraphs 13-28
[142] paragraphs 42-59
ILO-OSH 2001[143]

## 5.5 Umoja wa Ulaya na CSR

Ushiriki wa E.U na CSR ilianza mwaka 1995 na kusainiwa kwa Azimio la Biashara la Ulaya kuhakikisha jamii hazitengwi katika maendeleo kutoka kwa wafanyabiashara.[144] Mwezi Machi 2000, kwenye Mkutano wa Baraza la Ulaya la Lisbon, viongozi wa E.U walifanya kazi maalum juu ya wajibu wa kampuni kwa uwajibikaji wa kijamii ili kutoa fursa sawa, ushirikishwaji wa kijamii na maendeleo endelevu.[145]

Lengo la kimkakati lililopitishwa katika Mkutano wa Wakuu wa Ulaya wa Lisbon ni uchumi wenye ushindani na nguvu unaotegemea maarifa, uwezo wa ukuaji wa uchumi endelevu na ajira nyingi na bora na mshikamano zaidi kwa jamii.[146] Umoja wa Ulaya umepitisha mkakati wa kukuza CSR na hatua tofauti zilianza mwaka 2001 na kupitishwa na Waraka wa Kijani (Green Paper) juu ya CSR.[147] Dhana na uwajibikaji kwa jamii imejumuisha kampuni kuunganisha masuala ya kijamii na mazingira katika shughuli zao za biashara na katika mwingiliano wao na wadau kwa hiari.[148]

Waraka unabainisha baadhi sifa za CSR ndani ya biashara, na vile vile katika jamii na viwango vya kimataifa; ni hiari; na inahusishwa na ubora wa jamii.

[144] European Parliament. (2010). European Parliament Resolution of 25 November 2010 on Corporate Social Responsibility in International Trade Agreements (2009/2201(INI). Available at: http://www.europarl.europa.eu/sides/getDoc.do?type=TA&language=EN&reference=P7-TA-2010-0446

[145] 52 European Council, Speech by the President Nicole Fontaine, Presidency Conclusions, EUR. PARL. DOC. (01/S-2000) para. 39 (2000), *available at* http://www.europarl.eu.int/bulletins/pdf/1s2000en.pdf

[146] Based on the strategic goal adopted at the European Summit of Lisbon in March 2000 of becoming by 2010

[147] COMMISSION OF THE EUROPEAN COMMUNITIES Brussels, 18.7.2001 COM(2001) 366 final GREEN PAPER Promoting a European framework for Corporate Social Responsibility, https://eur-lex.europa.eu/LexUriServ/LexUriServ.do?uri=COM:2001:0366:FIN:EN:PDF%20

[148] Document 52011DC0681 COMMUNICATION FROM THE COMMISSION TO THE EUROPEAN PARLIAMENT, THE COUNCIL, THE EUROPEAN ECONOMIC AND SOCIAL COMMITTEE AND THE COMMITTEE OF THE REGIONS A renewed EU strategy 2011-14 for Corporate Social Responsibility /* COM/2011/0681 final */

Aidha ufafanuzi na sifa za CSR zilizoelezwa katika waraka huo, zinakuza mfumo wa wajibu wa Shirika au Kampuni kwa Jamii na inatambua umuhimu wa kusambaza na kushirikiana vizuri katika CSR. [149]

Katika kiwango cha biashara, sekta ambazo CSR inahusika ni pamoja na rasilimali watu, usimamizi, usalama na afya kazini, urekebishaji wa kampuni, na kusimamia athari za kampuni kwenye mazingira na maliasili.[150] Kwa upande wa mambo ya nje ya CSR inahusisha washirika wa kibiashara na wauzaji, wateja, jamii, taasisi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Waraka wa Kijani unabainisha ushirikiano wa kibiashara kwa wauzaji na watumiaji, haki za binadamu na mazingira.[151]

### 5.5.1 Mkakati wa Ulaya wa kukuza CSR

Mkakati wa Ulaya kukuza CSR unazingatia hiari katika kutekeleza CSR, uaminifu na uwazi, ushiriki wa SMEs na msaada kwa vyombo vilivyopo vya kimataifa vinavyohusiana na CSR.[152] Mkakati huo unajumuisha kuimarisha utaalam juu ya athari za CSR kwenye faida na ushindani;[153] kusambaza na kubadilishana uzoefu miongoni mwa SMEs na maeneo husika; na kuunganisha

[149] DIRECTIVE 2014/95/EU OF THE EUROPEAN PARLIAMENT AND OF THE COUNCIL of 22 October 2014 amending Directive 2013/34/EU as regards disclosure of non-financial and diversity information by certain large undertakings and groups

[150] 2.1.2 paragraph 31-34, Green Paper

[151] Published on 23 February 2022, the proposal for a New Directive on "Corporate Sustainability Due Diligence and amending Directive (EU) 2019/1937" is aiming to foster sustainable and responsible corporate behaviour throughout global value chains, https://www.clydeco.com/en/insights/2022/05/eu-directive-on-corporate-sustainability-due-dilig

[152] OECD : Miongozo ya Biashara za Kimataifa na viwango vya kimataifa vya kazi vilivyomo Mikataba ya kimsingi ya ILO).

[153] European Parliament. (2010). European Parliament Resolution of 25 November 2010 on Corporate Social Responsibility in International Trade Agreements (2009/2201(INI). https://eur-lex.europa.eu/legal-content/EN/TXT/?uri=CELEX%3A52010IP0446

watu na uwazi; kuunganisha CSR katika sera za Umoja wa Ulaya na kuweka viwango vya sera za kitaifa ili kuimarisha umoja.[154]

## 5.6 Mkataba wa AfCFTA[155]

Utekelezaji wa CSR wa bara la Afrika ni kama kielelezo cha usimamizi wa biashara na kusisitiza umuhimu wa CSR kwa mjadala wa maendeleo endelevu katika Afrika.[156]

Makubaliano ya AfCFTA na utekelezaji wake wa CSR unalenga kukuza utekelezaji na ushirikiano wa kikanda,[157] ingawa mkataba wa AfCFTA unapunguza uzito wa mpango wa ushirikiano wa Afrika kuelekea kufikia malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) barani Afrika[158]Kama ilivyooneshwa katika kifungu cha 8 ya Mkataba wa AfCFTA, itifaki zake na zinazohusiana na viambatanisho vinaunda sehemu muhimu ya makubaliano, hivyo, biashara na lengo la soko huria kwa biashara vitafutiwe utaratibu zaidi.[159]

Mkataba wa AfCFTA, una maeneo ambayo yanahusiana na uwajibikaji kwa jamii kwa kuhamasisha uwazi kwa kutaka kila nchi mwanachama kuchapisha au kutoa hadharani sheria zake, kanuni, taratibu na maamuzi ya kiutawala, chini ya makubaliano ya kimataifa yanayohusiana na biashara.[160]

---

[154] Mawasiliano kuhusu Wajibu wa Shirika kwa Jamii: Mchango wa biashara kwa Maendeleo Endelevu (2002) inawasilisha mkakati wa EU wa kukuza CSR.

[155] African Union (2018). Agreement Establishing the African Continental Free Trade Area March. Available at https:// au.int/en/treaties/agreement-establishing-african-continental-free-trade-area

[156] AGREEMENT ESTABLISHING THE AFRICAN CONTINENTAL FREE TRADE AREA, Assembly/AU/Dec. 569(XXV); https://au.int/sites/default/files/treaties/36437-treaty-consolidated_text_on_cfta_-_en.pdf

[157] Kifungu cha 14

[158] Uwafiokun Idemudia, 'Corporate Social Responsibility and Development in Africa: Issues and Possibilities' (2014) 8/7 Geography Compass 421; Douglas Branson, 'Corporate Governance "Reform" and the New Corporate Social Responsibility' (2001) 62 University of Pittsburgh Law Review 605, 606.

[159] kwa mujibu wa kifungu cha 3

[160] Kifungu cha 16 cha Mkataba

Mkataba wa AfCFTA na nyanja za kijamii na kiuchumi za maendeleo endelevu zinaonekana katika lengo lake mahususi katika kulenga kusaidia jamii na wananchi.[161] Kifungu hicho kinaeleza kukuza biashara ya bidhaa za ndani ya Afrika kupitia kuimarishwa kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, na ukuaji wa viwanda kote Afrika.[162] Matumizi ya utaratibu huu yanaweza kuruhusu uundaji na upitishaji wa chombo cha ziada cha kisheria kuhusu ushirikiano wa biashara, mazingira na ujenzi wa maendeleo endelevu kwa Afrika.[163]

## 5.7 Agenda 2063 na biashara

Ujumuishaji wa biashara ni sehemu muhimu ya Ajenda 2063 na Mpango wa Umoja wa Afrika wa miaka 50 kwa ajili ya mabadiliko ya Afrika kimuundo na mkakati wa pamoja mfumo shirikishi na endelevu maendeleo ambayo yanahusishwa na SDGs.[164]

2063 ina sehemu tatu kuu: maono ya 2063, mfumo wa mabadiliko, na hatua za utekelezaji, ufuatiliaji na mipango ya tathmini, ufadhili, mawasiliano mkakati na uwezo wa utekelezaji.

[161] Kifungu 2(1) na 2(2)(f), the AfCFTA Agreement (art.2(1)), and the social and economic facets of sustainable development appear in its specific objective in art. 2(2)(f), "to boost intra-African trade in goods through … enhanced socio-economic development, diversification and industrialisation across Africa.". These form an integral part of the AfCFTA Agreement once they are adopted.

[162] African Union (2011). Decision on Boosting Intra-African Trade and Fast Tracking the Continental Free Trade Area (Assembly/AU/Dec.394 (XVIII)). Available at https://au.int/sites/default/files/documents/32454-docdecision_-_english.pdf

[163] Judy Muthuri, 'Corporate Social Responsibility in Africa: Definition, Issues and Process' in R.T. Lituchy, B.J. Punnett and B.B. Puplampu (eds.), Management in Africa: Macro and Micro Perspective (New York and London: Routledge, 2013) 90–111

[164] Following intensive consultations and preparation, the African Union (AU) policy organs finally adopted the third document of Agenda 2063, the First Ten-Year Implementation Plan, in June 2015, in South Africa

Dira ya Ajenda 2063 ina matarajio saba yanayojumuisha Afrika yenye mafanikio yenye msingi wa ukuaji shirikishi na maendeleo endelevu na bara jumuishi, lenye umoja wa kisiasa, kwa kuzingatia maadili maono ya mwamko wa Afrika.[165] Malengo haya yanatambua mabadiliko ya uchumi, kilimo cha kisasa, uchumi wa bahari kwa ukuaji wa kasi wa uchumi, na endelevu kwa mazingira na inayostahimili hali ya hewa, na uchumi na jamii.[166]

## 5.8 Uzoefu wa nchi mbalimbali

### 5.8.1 Tanzania

Katika jitihada za kuimarisha eneo la CSR, mwaka 2002, Serikali ya Tanzania ilipitisha Sheria ya Kampuni ya 2002[167] iliyofuta Sheria ya zamani ya Kampuni ya 1932. Sheria ilijumuisha maendeleo ya kimataifa katika sheria ya ndani na kuweka taratibu za uwazi, utawala bora na majukumu ya mkurugenzi. Kiujumla Sheria kuu zinazohusiana na ushirikishwaji kwa jamii ni Sheria ya Kampuni, Sura ya 212 na Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya 1994.

### 1. Sheria ya Kampuni Nam. 12 ya mwaka 2002 [Cap.212, R.E 2002]

Sheria hii imeeleza maeneo mbalimbali ambayo yanaonesha uwajibikaji kwa jamii na yanajumuisha dhana hiyo ikiwemo**:**

---

[165] AGENDA 2063 FIRST TEN-YEAR IMPLEMENTATION PLAN 2014-2023, https://wedocs.unep.org/bitstream/handle/20.500.11822/20823/Agenda%202063%20-%20FIRST%20TEN%20YEAR%20PLAN%20%20%20September%20%202015.pdf?sequence=1&isAllowed=y

[166] Agenda 2063, The Africa We Want, "A shared strategic framework for inclusive growth and sustainable Development & a global strategy to optimize the use of Africa's Resources for the benefit of all Africans" published final in 2017, inapatikana https://au.int/sites/default/files/documents/33126-doc-01_background_note.pdf

[167] Correctly cited as Companies Act No. 12 of 2002

### (a) Uwazi

Mkurugenzi wa kampuni anapotekeleza majukumu yake anatakiwa kuwa na uaminifu na kwa nia njema na kwa kile anachoamini kuwa ni maslahi bora ya kampuni.[168] Kufichua kila taarifa inayowezekana kwa wanahisa kuhusu maslahi ya kampuni.[169] Kwa ujumla, Sura ya VII ya Sheria inatoa wajibu na madeni ya Wakurugenzi. Kwa kwa mfano, Kifungu cha 183 (1) kinatoa jukumu wakurugenzi wa kampuni kuzingatia katika utendaji wa majukumu yao, maslahi ya wanachama, wafanyakazi wa kampuni na wadau.[170]

### (b) Uadilifu

Kampuni lazima izingatie haki katika kulinda haki za wanahisa, pamoja na kutoa usuluhishi na ufanisi na akishindwa anatakiwa kuwajibishwa.[171] Masuala ambayo wakurugenzi wa kampuni wanapaswa kuzingatia katika utendaji wa majukumu yao ni maslahi ya wanachama, na maslahi ya wafanyakazi wa kampuni. Mkurugenzi ana jukumu la kutumia utaalamu, ujuzi na bidii ambayo ingetekelezwa katika mazingira sawa na anatarajiwa kutumia uzoefu alionao.[172]

Hii inajumuisha mchakato wa kufanya maamuzi inayohusisha ajira, ulinzi wa mazingira, maslahi ya jinsia, haki za watoto na haki za makundi yaliyo hatarini katika jamii.

[168] Kifungu 181, and 182 of the Company"s Act [Cap.212, R.E 2002]
[169] Kifungu 195 of Company"s Act [Cap.212, R.E 2002
[170] Vertigans, S, et al (2016). Corporate Social Responsibility in Sub Saharan Africa; Sustainable development in its embryonic form; Sprinter, Switzerland. Page 113
[171] Kifungu 383, 384 and 233 of the Company"s Act
[172] Kifungu 185 of Company"s Act [Cap.212, R.E 2002]

### (c) Uwajibikaji

Kampuni lazima ihakikishe kuwa Bodi inawajibika kwa wanahisa. Uwajibikaji inajumuisha mali na vitendo vya kampuni, kuwajibika kwa wanahisa na wadau wengine kwa maamuzi na vitendo vyake na katika kuzingatia maslahi halali na matarajio ya wadau wote.[173]

## 2. Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Nam. 5 ya 1994

Sheria hii inaanzisha Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa madhumuni ya kukuza na kuwezesha maendeleo kwa kufuata taratibu, haki na ufanisi katika soko la mitaji na dhamana nchini Tanzania, na kuweka masharti kuhusu soko la hisa, madalali na watu wengine wanaohusika na dhamana, na kwa madhumuni yaliyounganishwa.

Sehemu ya IX ya Sheria inakataza tabia kama vile kuunda biashara na masoko ya uongo, shughuli za wizi na udanganyifu katika soko. Matumizi ya shughuli au vifaa vya kuongeza au kukandamiza au kusababisha mabadiliko katika soko na bei dhamana.[174] ambayo adhabu yake ni kulipa faini isiyopungua Shilingi milioni tano au kifungo kwa muda usiopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja faini na kifungo.[175] Fidia zaidi inaweza kulipwa kwa hasara itakayothibitishwa na mtu kudai fidia.[176]

---

[173] Kifungu 376, 377, 378, and 380 of the Company‟s Act
[174] Kifungu 106 of the Capital Markets and Securities Act No. 5 of 1994
[175] Kifungu 113 of the Capital Markets and Securities Act No. 5 of 1994
[176] Kifungu 113 (1)(2) & (3) of the Capital Markets and Securities Act No. 5 of 1994

Hii inaonesha kwamba shughuli zozote za Kampuni nchini Tanzania lazima zizingatie Kanuni za Uwajibikaji kwa Jamii kwa sababu vitendo vya taaifa za uongo katika biashara, shughuli za wizi wa soko na udanganyifu zinaweza kuleta uusmbufu kwa umma kuhusu bei na matumizi ya bidhaa au bidhaa zinazouzwa.

### 3. Sheria ya Ardhi ya Kijiji[177]

Sheria hii inaeleza kwamba hakuna uhamisho wa ardhi ya kijiji utakaohamishwa kutokana na uwekezaji wa aina yoyote bila ya kutolewa fidia iliyokubaliwa kwa vipande vya ardhi kwa madhumuni ya uwekezaji. Ili kuepusha mgongano wa kimaslahi kati ya wanakijiji na Kampuni, Sheria ya Ardhi ya Kijiji inatoa nafasi ya kulipa fidia. Sheria imeweka kosa kwa kughushi ripoti ya tathmini ya athari kwa mazingira baada ya utafiti ili kuhakikisha kwamba kampuni za uwekezaji zinazingatia tathmini ya athari ya mazingira na kanuni za ukaguzi.[178]

### 4. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (EMA) Nam. 20 ya mwaka 2004

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira EMA inazitaka kampuni kuwasilisha tathmini ya athari za mazingira (EIA) pamoja na mpango wa usimamizi wa mazingira (EMP), kabla ya kuanza shughuli zake.[179] Aidha, Sheria inazitaka kampuni kudhibiti na kuzuia uchafuzi wa mazingira, kudhibiti bidhaa taka, na imefanikiwa kuweka vifungu vya adhabu kwa kushindwa kuzingatia masharti hayo na kushirikisha wananchi katika tathmini hiyo.[180] Sheria imeweka

[177] No 5 of 1999
[178] Kifungu cha 60
[179] Sehemu ya Sita (kifungu 81-103)
[180] Kifungu cha 89

masharti ya kupatiwa elimu wananchi na kushirikishwa katika kudhibiti uharibifu wa mazingira.[181]

5. **Sheria ya Petroli Nam. 8 ya mwaka 2015[182]**

Sheria ya Mafuta -Petroli inaweka utaratibu wa udhibiti wa shughuli za mafuta ya petroli juu ya mkondo wa kati na chini na kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli. Sehemu ya VIII ya Sheria inahusu ushiriki wa Serikali, ambayo imeweka wajibu wa Kampuni kwa Jamii pamoja na ahadi ya uadilifu.[183]

Aidha, Kifungu cha 223 cha Sheria kinatoa Wajibu wa Kampuni kwa Jamii na kuzitaka kutayarisha mpango unaoaminika wa uwajibikaji wa kijamii pamoja na mamlaka husika za Serikali za mitaa. Mpango huo utazingatia shughuli za kimazingira, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni na kuwasilishwa mamlaka ya Serikali ya mtaa kwa ajili ya kuzingatiwa na kuidhinishwa. Aidha Sheria imeweka adhabu kwa mtu atakayekiuka agizo lolote lililotolewa chini ya Sheria hii atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni mia tano.[184]

6. **Sheria ya Madini ya Tanzania Nam. 14 ya mwaka 2010**

Sheria ya Madini ya Tanzania, inatamka wazi chini ya Kifungu cha 10 cha Mkataba wa Maendeleo ambao Waziri anaingia kwa niaba ya Serikali. Mkataba

[181] Kfungu cha 178
[182] No. 8 of 2015
[183] Sehemu ya VIII
[184] kifungu cha 239(b)

unahakikisha utekelezwaji wa mradi wa CSR kwa kampuni husika kama ilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 10(4) ingawa ushurutishaji wake hautaji CSR moja kwa moja.[185]

### 5.8.2 Kenya

1. **Sheria ya Makampuni ya 2009, na sheria ya Masoko ya Mitaji (CMA)**

#### (a) Uwajibikaji

Sheria ya Kampuni inaeleza kwamba wakurugenzi wanawajibika kibinafsi kwa taarifa za uongo katika maelezo ya kampuni.[186] Kuhusu Miongozo ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji (CMA), inaeleza kwamba kila kampuni ya umma iliyoorodheshwa inapaswa kuongozwa na bodi yenye ufanisi na kutoa mwongozo wa kimkakati, kuongoza na kudhibiti kampuni na kuwajibika kwa wanahisa wake.[187]

#### (b) Uadilifu

Miongozo ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji (CMA) inatoa muundo wa bodi na pia utaratibu wa uwakilishi wa walio wachache bila kuathiri uwajibikaji wa pamoja wa wakurugenzi.[188] Miongozo pia inashughulikia kiwango cha umiliki wa kigeni, [189] na muundo wa bodi pia unapaswa kutoa utaratibu wa uwakilishi ya wanahisa wachache.[190] Mwongozo unahitaji kila kampuni ya umma iliyoorodheshwa kutenganisha nafasi ya mwenyekiti na mtendaji mkuu ili kuhakikisha uwiano wa mamlaka.[191]

---

[185] Kifungu cha 10
[186] Kifungu 45 of the Companies Act of 2009
[187]The CMSA Guidelines at 2.1.
[188] Paragraph 3.1.2 (iii) of the CMA guidelines
[189] The CMA Guidelines at 3.3 (i).
[190] Guidelines Paragraph 3.1.2(iii)
[191] Guidelines at 3.2 (i) & (ii).

### (c) Uwazi

Kifungu cha 31 (3) kinaeleza kwamba Vyama vya wafanyakazi lazima, kupitia Tume na chini ya masharti kama yatakavyoamuliwa na Tume, vipewe idhini ya kufikia taarifa za fedha za kampuni kwa madhumuni ya kufuatilia mchakato wa biashara.[192] Pia kama bodi itatoa msaada wa kifedha kwa mkurugenzi au afisa ni lazima itoe taarifa ya maandishi kwa wanahisa wote na kwa biashara yoyote.[193]

## 2. Sheria ya Soko la Hisa (SURA 485A)

Kuhusu Wajibu wa Shirika kwa Jamii, ndani ya Sheria ya Soko la Mitaji, inafafanua utawala bora kama, mchakato na muundo uliotumika kuelekeza na kusimamia masuala ya biashara ya kampuni kuelekea kuimarisha ustawi na uhasibu wa Kampuni kwa lengo kuu la kutambua thamani ya mwisho ya mwenye hisa huku akizingatia maslahi ya wadau wengine.[194]

Sheria hii pia inaweka uwiano kati ya Mashirika ya kiuchumi, malengo ya kijamii na ya jumuiya na kutia moyo matumizi bora ya rasilimali, uwajibikaji katika matumizi ya madaraka.[195]

[192] The Companies Act of 2009
[193] Kifungu 45(5) of the Companies Act of 2009
[194] CAP. 485A: Guidelines on Corporate Governance Practices by Public Listed Companies In Kenya. Gazette Notice No. 3362, Kifungu 1.2
[195] Kifungu 1 of the Capital Market Act (CAP. 485A)

### 3. Sera ya Chuo cha Mafunzo ya Afya KMTC[196] juu ya Uwajibikaji wa Wawekezaji kwa Jamii 2019

Sera hii ni sera ya chuo cha mafunzo juu ya masuala ya afya Kenya ambayo taasisi hiyo imejiwekea kama ni muongozo wao katika kutekeleza wajibu wao kwa jamii kupitia malengo yao makuu yafuatayo:[197]

(a) Kuhakikisha wadau wote wanafahamishwa kikamilifu kuhusu shughuli za Wajibu wa Wawekezaji kwa Jamii za Chuo hicho.

(b) Kutoa usaidizi wa kimatibabu kwa kutangaza huduma za afya ya kinga kupitia utafiti na machapisho na pia kutayarisha kambi za matibabu ili kutoa matibabu kwa jamii zinazoishi karibu na vyuo hivyo.

(c) Kuhakikisha uendelevu wa mazingira kwa kupanda miti pamoja na mipango mingine ya kuhifadhi mazingira, kufanya utafiti na kampeni za uhamasishaji juu ya uendelevu wa mazingira.

(d) Kusaidia utoaji wa elimu kwa wahitaji kwa kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wenye uhitaji nchini Kenya kupitia kuanzishwa kwa program ya amana ya elimu.

(e) Kushiriki katika juhudi za kukabiliana na maafa ndani na nje ya kampasi zake na maeneo mengine ya Nchi.

Aidha mikakati ya utekelezaji wa Sera hii imegaiwa katika maeneo elimu, uhifadhi wa mazingira, masuala ya afya, kupambana na majanga na misaada ya mahitaji ya lazima kwa Jamii.

---

[196] Kenya medical training collage inapatikana https://kmtc.ac.ke/wp-content/uploads/2019/06/10.-KMTC-Corporate-Social-Responsibility-Policy.pdf

[197] vifungu 1.4 na 1.5 vya Sera

### 5.8.3 UGANDA

Sheria zinazohusiana na uwajibikaji wa kampuni kwa jamii unasimamiwa na Sheria ya Kampuni, Sura ya 110 ya mwaka 2012, Miongozo ya Utawala Bora wa Mashirika ya Masoko ya mwaka 2003, na Sheria ya Mamlaka ya Soko la Mitaji ya 1996 Sura ya 84, R.E 2000.

**(a) Uwajibikaji**

Kanuni ya 6 ya Miongozo ya Utawala Bora inatoa malengo ya Miongozo ambayo ni kuimarisha utawala wa shirika na kampuni na kukuza viwango vya udhibiti katika kampuni nyengine za umma ili kuwa na kiwango cha utawala kulingana na mwelekeo wa kimataifa.[198] Miongozo inataka kila kampuni iliyoorodheshwa kutekeleza misingi ya utawala bora kama sehemu ya kuendeleza majukumu yao.[199]

Aidha sheria ya Mitaji ya Umma katika kifungu cha 7 na 84 inataka uwajibikaji kwa mtu yeyote ambaye kwa makusudi anatoa taarifa za uongo,[200] kufanya miamala ya uwongo ya biashara na wizi wa soko,[201] na kughushi kumbukumbu.[202]

**(b) Uadilifu**

Miongozo inatoa haki, kwamba; muundo wa Bodi unapaswa kuakisi muundo wa uhisani wa kampuni na haipaswi kuwa na upendeleo. Zaidi ya hayo,

[198] Capital Markets Corporate Governance Guidelines of 2003
[199] Rule 8 of the Capital Markets Corporate Governance Guidelines of 2003
[200] The Capital Market Authority Act of 1996 Cap.84, R.E 2000
[201] Kifungu 82 of the Capital Market Authority Act of 1996 Cap.84, R.E 2000
[202] Kifungu 95 of the Capital Market Authority Act of 1996 Cap.84, R.E 2000

inapaswa kuwa na kipengele cha uwakilishi wa wanahisa wachache.[203] Kifungu cha 247 cha Sheia ya Kampuni katika eneo hili, kimetoa haki kwa walio wachache kuhusu kitendo chochote kisicho cha haki iliyotendwa dhidi yao na kampuni,[204]

**(c) Usawa**

Bodi ya Wakurugenzi inapaswa kuakisi usawa katika utendaji na kuhakikisha kuwa hakuna mtu binafsi au kikundi cha watu binafsi kinachotawala michakato ya kufanya maamuzi ya bodi.[205] Sheria inaeleza kwamba wakurugenzi watafanya kazi kwa njia ambayo inakuza mafanikio ya biashara ya kampuni na kutumia utaalam katika kukuza biashara.[206]

**(d) Uwazi**

Miongozo inatoa wajibu wa kutoa taarifa katika ripoti za mwaka za shirika na ufichuzi wa maeneo yote ya kutofuata sheria mbadala.[207] Uwazi pia umeelezewa katika sheria ya kampuni kuhusu wajibu wa mkurugenzi kufichua malipo ya upotezaji wa ofisi, yaliyofanywa kuhusiana na kuchukua au kuhamisha hisa katika kampuni.[208]

**(e) Wajibu wa Kampuni kwa Jamii**

Kanuni za Mitaji ya Umma zinataka Wajumbe wa bodi kutenga muda wa kutosha kutekeleza majukumu yao na kushughulikia wanahisa wote na

[203] Rule 14, 17 and 40 of the Capital Markets Corporate Governance Guidelines of 2003
[204] The Companies Act, Cap.110 of 2012
[205] Rule 15 of the Capital Markets Corporate Governance Guidelines of 2003
[206] Kifungu 198 of the Companies Act, Cap.110 of 2012
[207] Rule 10 of the Capital Markets Corporate Governance Guidelines of 2003
[208] Kifungu 213 of the Companies Act, Cap.110 of 2012

kutambua fursa za biashara za ushirika pamoja na athari katika mazingira ya uendeshaji ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa sahihi, hatua za kudhibiti hatari kama hizo au mabadiliko yanayotarajiwa yanayoathiri Kampuni.[209]

Hii ni kuhakikisha kwamba chochote kinachofanywa na hufanya lazima kuzingatia athari za mazingira ambazo zinaweza kutokea wakati wa utekelezaji wa shughuli za biashara na kuimarisha utekelezaji wa hatua zinazofaa kudhibiti hatari kama hizo au mabadiliko yanayotarajiwa kuleta athari.

### 5.8.4 Philiphines

#### (a) Sheria ya Uwajibikaji wa Wawekezaji kwa Jamii Senate S.B. No. 1239

Sheria ya Uwajibikaji wa Wawekezaji kwa Jamii kupitia Sheria ya Uwajibikaji wa Wawekezaji kwa Jamii ya Philiphines imelenga kuhimiza maendeleo endelevu ya kiuchumi na hifadhi ya mazingira. Sheria ya Uwajibikaji kwa Jamii inatangaza kwamba Serikali inatambua jukumu muhimu la sekta ya kibinafsi katika ujenzi wa taifa na itahimiza ushiriki wake wa dhati katika kukuza maendeleo ya kiuchumi na ulinzi wa mazingira nchini.[210]

Aidha, miongoni mwa mambo mengine muhimu yaliyozingatiwa katika sheria hiyo ni pamoja na kuweka utaratibu wa uwajibikaji wa kisheria kwa mashirika, mashirika hayo yawe ya ndani au kutoka nje ya utawala wa ufilipino, ubia baina ya serikali ya ufilipino na taasisi nyengine zinazofanya biashara nchini humo.

---

[209] Rule 14 of the Capital Markets Corporate Governance Guidelines of 2003

[210] An Act Institutionalizing Corporate Social Responsibility, Providing Incentives Therefor, and for Other Purposes, Fifteenth Congress Of The Republic of the Philippines First Regular Session, SENATE S.B. No. 1239

Vile vile katika sheria hiyo, mashirika yote ya biashara yamepewa jukumu la kuzingatia maslahi ya jamii kwa kuwajibika kwa athari zote zitakazotokana na shughuli zao kwa upande wa wateja, wafanyakazi, wanahisa na wanajamii kwa ujumla.

Miongoni mwa vipengele muhimu vya sheria hiyo ni pamoja na Tamko la Sera la Serikali kutambua wajibu muhimu kwa sekta binafsi katika ujenzi wa taifa na na uimarishaji wa uwajibikaji wa wawekezaji kwa kijamii kupitia mashirika yote ya biashara,[211] Wajibu wa Wawekezaji kwa Jamii, [212] upatikanaji wa mapato na gharama,[213] Ripoti za vipindi maalum kuhusu utekelezaji wa CSR,[214] na wajibu wa kutekeleza wa sheria na kanuni mbalimbali.[215]

### (b) Sheria ya Kuanzisha Wajibu Wa Kijamii kwa Walipa Kodi Wakubwa Nam. 2747[216]

Sheria hii inatoa jukumu kwa Shirika la kijamii, Mashirika yote makubwa ya walipa kodi, yawe ya ndani au nje, yanafanya biashara nchini, yana mamlaka ya kutenga asilimia ya kutosha ya mapato yao halisi kwa uwajibikaji wa shirika kwa jamii (CSR).[217]

Kwa madhumuni ya Sheria hii wajibu wa kampuni au shirika kwa jamii imetafsiriwa kama kujitolea kwa biashara kuwa na maadili na kuchangia

[211] Kifungu cha 2
[212] Kifungu cha 3,
[213] Kifungu cha 4
[214] Kifungu cha 5
[215] Kifungu cha 6
[216] An Act Institutionalizing Corporate Social Responsibility among Large Tax Payers and Providing Incentives Therefor 2747
[217] Kifungu cha 3

uchumi endelevu, maendeleo kwa kufanya kazi na wadau husika ili kuboresha maisha yao kwa njia ambazo ni nzuri kwa biashara, ajenda ya maendeleo endelevu na jamii kwa ujumla.[218] Kwa mujibu wa kifungu cha 3, shughuli zinazohusiana na CSR zitajumuisha misaada; masuala ya kisayansi; maendeleo ya vijana na michezo; masuala ya kitamaduni au elimu; huduma kwa wastaafu na wazee; ustawi wa jamii; uendelevu wa mazingira; afya; na msaada na usaidizi wakati wa maafa.

Aidha katika kukamilisha lengo la CSR, Vitengo vya Serikali za Mitaa na taasisi zote za Serikali zitatoa msaada wowote unaohitajika na mashirika makubwa ya walipa kodi katika utekelezaji wao wa CSR.[219] Sheria imetoa wajibu wa kutayarisha ripoti za mara kwa mara kama sehemu ya ripoti yake ya kila mwaka kwa Tume inayoshughulikia masuala ya Hisa na Mitaji (Securities and Exchange Commision) na orodha ya shughuli zinazohusiana na uwajibikaji wao wa kijamii wa shirika.[220]

### 5.8.5 Afrika Kusini

Mfumo wa uwajibikaji kwa jamii CSR nchini Afrika Kusini, unasimamiwa na Katiba, Sheria ya BBBEE, Sheria ya Makampuni ya 2008 na sheria ya Ajira (EEA). Sheria hizi ni baadhi ya sheria ambazo Serikali ya Afrika Kusini ilitangazwa ili kuhakikisha kuwa biashara zinazingatia masuala ya kijamii, kimazingira na kiuchumi.

[218] Ibid kifungu cha 3
[219] Kifungu cha 5
[220] Kifungu cha 6

## 1. Katiba ya Jamhuri ya Afrika Kusini 1996[221]

Katiba inajumuisha Mswada wa Haki (Bill of Rights) na imetoa haki mbalimbali kwa ajili ya raia wa Afrika Kusini. Katiba inasisitiza haki za watu wote katika nchi na inathibitisha maadili ya kidemokrasia ya utu, usawa na uhuru wa binadamu.[222] Kwa hivyo Mswada wa Haki unapaswa kuchukuliwa kwa uzito mkubwa kwa kadiri matumizi yake yanavyohusika kwa msingi wa demokrasia nchini Afrika Kusini.

Kifungu cha 8(2) cha Katiba kinataka kila mtu kuzingatia haki kwa kiwango ambacho, itatumika, kwa kuzingatia asili ya haki inayodaiwa na wajibu wowote uliowekwa kisheria.

## 2. The Broad-Based Black Economic Empowerment Act (the BBBEE Act), the 2008

Sheria hii ilitungwa kuhakikisha umiliki wa watu weusi kwa baadhi ya mashirika makubwa ya viwanda nchini. Sera ya Uwezeshaji Weusi Kiuchumi (BEE) ililenga kuongeza hisa ya umiliki wa watu weusi katika kampuni kubwa ya Afrika Kusini.[223]

Lengo pana la Sheria hiyo lilikuwa kupunguza tatizo la ukosefu wa usawa wa utawala wa ubaguzi wa rangi kwa kugawa upya kisheria jumuiya ya watu weusi na kuleta mchanganyiko sehemu za kazi kupitia ukuzaji utaalam na mafunzo na kwa ujumla kukuza maendeleo ya watu weusi.[224]

---

[221] The South African Constitution, No 108 of 1996

[222] Kifungu cha 7(1)

[223] Croucher, R. and Miles, L. 2010. Corporate Governance and Employees in South Africa. Journal of Corporate Law Studies, 10 (2): 367-389.

[224] Babarinde, O. A. 2009. Bridging the economic divide in the Republic of South Africa: A corporate social responsibility perspective. Thunderbird International Business Review, 51 (4): 355-368., ukurasa 361

Sheria ya Uwezeshaji Watu Weusi Kiuchumi (BBBEE) ilitungwa kwa mara ya kwanza mwaka 2003, na ilirekebishwa baadaye mwaka wa 2013 na sasa inajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Uwezeshaji Weusi Kiuchumi, (BBBEE) 2013.[225] Marekebisho yalilenga uzingatiaji wa Sheria kwa vyombo vya dola na mashirika ya serikali, pamoja na marekebisho ya vyombo vya serikali na mashirika ya serikali kulazimika masharti hayo.[226]

Aidha Sheria, pia imeruhusu tathmini na ufuatiliaji sahihi wa kufuata; kuunda mipango ya motisha ili kusaidia kampuni ya biashara zinazomilikiwa na kusimamiwa na weusi. Sheria imeweka masharti ya kufutwa kwa mkataba au idhini pale ilipodhihirika kuwa mkandarasi hakuwa katika kufuata Sheria; na kuanzisha Tume ya Uwezeshaji Watu Weusi Kiuchumi, ambayo ilipewa jukumu la kushughulikia masuala yanayohusiana na kufuata Sheria ya BBBEE iliyorekebishwa, ilishughulikia masuala ya umiliki wa shirika, usimamizi, usawa mahali pa kazi, ukuzaji wa utaalam, na vile vile, ununuzi wa upendeleo na maendeleo ya biashara.[227]

Sheria ya BBBEE inazitaka kampuni kuunda kadi ya matokeo ambayo itaendeleza jinsi gani kampuni ilikuwa kubadilisha inaweza kupimwa.[228] Kila kampuni inatarajiwa kuweka malengo yake kuhusu vipengele vya kadi ya alama, ambapo maendeleo kwenye mabadiliko yanaweza kufuatiliwa na kampuni au na chama chochote huru.[229]

[225] B-BBEE Act, No. 53 of 2003.
[226] Kifungu cha 3
[227] Kifungu cha 3
[228] Kifungu cha 7
[229] Kifungu cha 7 na 8

Sheria ya BBBEE inaonekana kama mchangiaji mkuu kwa utekelezaji wa CSR ya kampuni. Sheria inaagiza kampuni kufanya uwekezaji wa kimkakati katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya watu waliokuwa hawana uwezo hapo awali kwa kuchangia mashirika ya kutoa misaada au kuhusika katika mipango mahususi ya tasnia ya kutoa misaada.[230]

### 3. Sheria ya Kampuni Nam. 71 ya mwaka 2008[231]

Sheria ya Kampuni na Kanuni za kampuni za mwaka 2011, zilianza kutumika tarehe 1 Mei 2011. Sheria hii imeleta mabadiliko ya kimsingi kwa sheria ya kampuni ya Afrika Kusini.[232] Lengo la Sheria hiyo, ni kupanua ushiriki wa wadau katika hatua za kampuni na kutoa mahitaji ya kuboresha udhibiti wa shughuli za kampuni, hasa katika maeneo ya uwajibikaji na uwazi.[233]

Kuhusu utekelezaji wa CSR, Sheria ilianzisha Kamati ya Kijamii na Maadili (SEC) ambazo huwezesha kampuni kusimamia wajibu wao wa kijamii na masuala ya wadau kwa uwajibikaji zaidi. [234] Kamati ya Kijamii na Maadili (SEC) chini ya kifungu cha 72 inajulikana kama Kamati ya Kijamii na Maadili (SEC). Kampuni zote zinazomilikiwa na serikali, kampuni ya umma zilizoorodheshwa na kampuni nyengine yoyote, na Waziri anaweza kuyaainisha hadharani maslahi ya kuwa na SEC ikilinganishwa na mchango kwa CSR. [235]

---

[230] Misingi na lengo la sharia kifungu cha 2 na 3
[231] The Companies Act No. 71 of 2008, as amended by the Companies Amendment Act No.3 of 2011 and the Companies Regulations (2011), came into effect on 1 May 2011
[232] KPMG. 2017b. King IV summary guide Available: https://assets.kpmg.com/content/dam/kpmg/za/pdf/2016/11/King-IV-SummaryGuide.pdf
[233] Ramlall, S. 2012. Corporate social responsibility in post-apartheid South Africa. Social Responsibility Journal, 8 (2): 270-288., ukurasa 280
[234] Kifungu cha 72
[235] Kifungu cha 72(4)

SEC imepewa uwezo wa kuhitaji maelezo kutoka kwa wakurugenzi au maafisa wa kampuni au mfanyakazi mwengine yeyote wa kampuni wakati wowote.[236]

## 4. The Employment Equity Amendment Act, No 47 of 2013 (EEA) The Employment Equity Act (EEA)

Sheria ya Usawa wa Ajira (EEA) ilikuwa jaribio la kisheria la Afrika Kusini la kuzuia vitendo visivyo vya haki na ubaguzi mahali pa kazi, hasa dhidi ya watu weusi na wasiojiweza hapo awali.[237]

EEA ilitungwa kwa mara ya kwanza mwaka 1998 na kurekebishwa kwa mara ya kwanza mnamo 2013 Sheria hii inatoa maana na maudhui ya haki ya usawa mahali pa kazi.[238] Lengo kuu likiwa ni kuondoa vikwazo vya ajira vinavyopatikana kwa wanachama wa vikundi vilivyoteuliwa. Pia ilitaka kuunda uwakilishi wa nguvu kazi, pamoja na kubadilisha sehemu ya kazi ya Afrika Kusini kuwa usawa mmoja zaidi na mwakilishi wa nchi.[239]

Sehemu ya 15 ya EEA inafafanua hatua za uthibitisho kama hatua muhimu ili kuhakikisha kwamba watu walio na sifa stahiki kutoka katika makundi maalum wanakuwa na fursa sawa na wanawakilishwa kwa usawa katika nyanja zote za kazi na viwango vya kazi vya mwajiri.[240] Aidha makundi yote kisheria yanaelezwa kama makundi yaliyoteuliwa kumaanisha watu weusi, wanawake

[236] Kifungu cha 72(3)
[237] Horwitz, F. M. and Jain, H. 2011. An assessment of employment equity and broad based black economic empowerment developments in South Africa. Equality, Diversity and Inclusion: An International Journal, 30 (4): 297-317., ukurasa wa 289
[238] Kifungu cha 6
[239] Kifungu cha 10 na kifungu cha 36
[240] Kifungu cha 15

na watu wenye ulemavu ambao ni raia wa Jamhuri na ambao walitengwa na sera za ubaguzi wa rangi.[241]

## 5. Miongozo na viwango vya usimamizi wa Kampuni na Mashirika vya Afrika Kusini "The King Reports – Codex" ya CSR

Miongozo na viwango vya usimamizi wa shirika vya Afrika Kusini vinawekwa kitaasisi na havijumuishi hati rasmi za kisheria; inachukuliwa kuwa miongozo ya hali ya juu ya utawala bora wa kampuni au shirika na kupitishwa kwake kunajulikana katika nyanja ya biashara ya nchi.

Mnamo 1994, Kamati ya Utawala Bora ilitoa ripoti ya kwanza, iliyolenga kukuza utawala wa ushirika na viwango vya kutosha kwa bodi ya wakurugenzi wa makampuni yaliyoorodheshwa, taasisi za fedha na baadhi ya makampuni ya umma. Huku ikihimiza utendaji wa utawala bora, ripoti hiyo pia ilisisitiza haja ya mashirika kuwajibika kijamii katika maeneo na jamii wanapofanyia kazi.[242]

Mnamo 2002, ripoti ya II juu ya Utawala wa Biashara ilichapishwa. Waraka wa pili uliweka wazi na kueleza vipengele saba vya utawala bora ambavyo shirika lolote linalopitisha ripoti hiyo linapaswa kuzingatia: nidhamu, uwazi, haki, uwajibikaji wa kijamii, uhuru, uwajibikaji na uwajibikaji.[243]

---

[241] Kifungu cha 1(b) cha sheria

[242] Sir Adrian Cadbury Corporate Governance Overview, 1999 World Bank Report 1. Corporate governance in South Africa was institutionalised by the publication of the King Report on Corporate Governance ("King Report 1994") in 1994, https://old.ecseonline.com/PDF/King%20Committee%20on%20Corporate%20Governance%20-%20Executive%20Summary%20of%20the%20King%20Report%202002.pdf, ukurasa wa 6

[243] King Committee on Corporate Governance, King Report on Corporate Governance for South Africa, 2002: King Report on Corporate Governance for South Africa 2002, King Committee on Corporate Governance

Toleo la Tatu lililorekebishwa la Kanuni na Ripoti ya Kanuni za Utawala wa Afrika Kusini au ripoti ya King III ilianza kutumika mwezi Machi 2010. Ripoti inazungumzia masuala ya uendelevu na vihatarishi (risk), huku ikiendelea kuangazia umuhimu kwa kampuni kuwasiliana na kujibu wadau wote. Ripoti imezingatia Uongozi wa kimaadili na uraia wa kampuni au shirika, bodi na wakurugenzi, kamati za ukaguzi, utawala wa hatari, utawala wa teknolojia ya habari, uzingatiaji wa sheria, kanuni, kanuni na viwango, ukaguzi wa ndani, usimamizi wa mahusiano ya wadau na jumuishi. kuripoti na kufichua.[244]

### 6. India Sheria ya Kampuni Nam. 18 ya mwaka 2013

Sheria inatoa jukumu kwa Bodi ya Wakurugenzi, baada ya kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya CSR, kupitisha sera ya CSR yaa Kampuni kuhusu CSR. Bodi lazima ihakikishe ni shughuli zile tu ambazo zimetajwa katika sera.

Bodi ya Wakurugenzi itahakikisha kwamba kampuni inatumia katika kila mwaka wa fedha, kiwango cha chini cha asilimia 2 ya wastani wa faida halisi iliyopatikana katika miaka 3 ya fedha iliyotangulia mara moja kulingana na sera ya CSR. Iwapo kampuni haijakamilisha miaka 3 ya kifedha tangu kuanzishwa kwake, wastani wa faida halisi itahesabiwa kwa miaka ya fedha tangu kuanzishwa kwake.[245]

Ripoti ya Bodi itaeleza Muundo wa Kamati ya CSR na kuingizwa katika Sera ya CSR. Ikiwa matumizi ya CSR hayafikii asilimia 2 kulingana na Sera ya CSR,

---

[244] Institute of Directors in Southern Africa, the King Report on Governance for South Africa 2009 https://cdn.ymaws.com/www.iodsa.co.za/resource/resmgr/king_iii/King_Report_on_Governance_fo.pdf
[245] Kifungu cha 135(4)

sababu za kiasi kisichotumika, na maelezo ya uhamishaji wa kiasi ambacho hakijatumika kinachohusiana na CSR inatakiwa kuelezwa na kuwekwa katika mfuko maalum (uhamisho ndani ya kipindi cha miezi sita kutoka kumalizika kwa mwaka wa fedha).[246]

Majukumu ya Kamati ya CSR ni kuunda na kupendekeza sera ya CSR kwa Bodi. Sera ya CSR itaonyesha shughuli zinazopaswa kufanywa na kampuni kama ilivyoorodheshwa katika sehemu ya VII.

Kamati ya CSR itapendekeza kiasi cha matumizi yatakayotumika kwa shughuli za CSR zitakazofanywa na kampuni, Kamati ya CSR itafuatilia sera ya CSR ya Kampuni mara kwa mara na Kamati itaweka utaratibu wa uwazi wa udhibiti wa utekelezaji wa miradi au programu au shughuli za CSR zinazofanywa na kampuni.[247]

## 7. Jamhuri ya Indonesia

### (a) Katiba ya Indonesi ya mwaka 1945[248]

Kifungu cha 33 cha Katiba ya msingi ya Indonesia, ambacho kilifanyiwa marekebisho mwaka wa 2002, kinahalalisha kuwa sekta zote za kiuchumi zinalenga kuleta ustawi kwa watu wa Indonesia, ambao ni pamoja na jamii za wenyeji.[249] Aidha kuhusiana na CSR, sheria zote za CSR zilizopitishwa na

[246]Kifungu cha 135(2)
[247] Kifungu cha 135(3)
[248] Undang-Undang Dasar 1945
[249] Schwartz, M. S., & Carroll, A. B. (2003). Corporate social responsibility: A three-domain approach. Business Ethics Quarterly, 13(4), 503-530. https://doi.org/10.5840/beq200313435

Serikali kuu na kanuni za utekelezaji zinategemea uwezo wa Kifungu cha 33 kuthibitisha serikali mamlaka juu ya maeneo ya maliasili.

### (b) Sheria ya Kampuni Nam. 40 ya mwaka 2007[250]

Sheria ya Kampuni ya Indonesia, inazitaka kampuni katika sekta za maliasili kutekeleza uwajibikaji wa kijamii na kimazingira.[251] Sheria ya Kampuni ina udhibiti wa utekelezaji kupitia Kanuni ya Serikali Nam. 47 ya mwaka 2012 kuhusu CSR. Kanuni hii ya utekelezaji inaelekeza bodi ya wakurugenzi katika kampuni kama mhusika mkuu ina wajibu kuhusiana na sheria hii; na inabainisha kuwa fedha hizo zinapaswa kutolewa kwa gharama za uendeshaji wa kampuni badala ya faida ya kampuni. Kwa Kampuni zinazomilikiwa na Serikali (SOC) Wizara imeweka Amri ya Mawaziri Nam. 08/MBU/2013 kuhusu Mpango wa Ubia na Ujenzi wa Mazingira kupitia fedha za asilimia 2 ya faida ya kampuni.

### (c) Sheria ya Mafuta na Gesi Nam. 22 ya mwaka 2001

Sheria hii haina kanuni muhimu za jinsi ya kutekeleza Maendeleo ya Jamii; badala yake, mwelekeo umetolewa katika eneo la urejeshaji gharama, kuthibitisha miradi na gharama wakati wa hatua ya uchunguzi (kabla ya uchimbaji na uzalishaji).[252]

---

[250] The Law of The Republic of Indonesia Number 40 of 2007, the Indonesia's Limited Liability Company Act (2007),

[251] Kifungu cha 74

[252] Kanuni ya Serikali Nam 79/ 2010

Miongozo zaidi ni kupitia chombo cha Udhibiti wa Mafuta na Gesi kwa shughuli za Mkondo wa Juu na Shughuli za Biashara ya Gesi, na kuelekeza programu za uwajibikaji kwa jamii katika maeneo ya afya, elimu, miundombinu, mazingira na uwezeshaji wa kiuchumi. Sheria hii pia imeweka adhabu kwa watakaokiuka sheria na taratibu.[253]

### (d) Sheria ya Mashirika yanayomilikiwa na Serikali Nam. 19 ya mwaka 2003

Sheria hii inasimamia Mashirika yanayomilikiwa na Serikali na wanaofaidika ni wajasiriamali wadogo, vyama vya ushirika, na jumuiya.[254] Sheria imeweka Mpango unaosimamiwa na kitengo chini ya bodi ya wakurugenzi ambao unatokana na asilimia 2 ya faida halisi ya SOC na Mpango huo unapaswa kuidhinishwa na wanahisa (Serikali Kuu).[255]

### (e) Sheria ya Uwekezaji Nam. 25 ya mwaka 2007

Sheria hii inazungumzia masharti ya uwekezaji na katika misingi na malengo imeainisha kuhamaissha maendeleo na kusaidia jamii.[256]

Sheria imetoa wajibu kwa kila mwekezaji kutumia kanuni ya utawala bora;[257]na kutekeleza uwajibikaji wa kijamii wa kampuni;[258] na kufuata masharti yote ya sheria na kanuni.[259] Aidha kifungu cha Uwajibikaji wa shirika kwa jamii umeelezwa katika kifungu hicho kinamaanisha jukumu lililowekwa

[253] Administrative sanctions (article 16).
[254] Kifungu cha 2
[255] Kifungu cha 36
[256] Kifungu cha 3(2)(f)na (h)
[257] Kifungu 15(a)
[258] Kifungu 15(b)
[259] Kifungu 15€

katika kila kampuni ya uwekezaji ili kuendelea kuunda uhusiano ambao unapatana, kwa usawa na unaofaa kwa ujirani, maadili, kanuni na utamaduni wa jumuiya ya karibu. Sheria inaweka vikwazo vya kiutawala katika mfumo wa onyo lililoandikwa kutoka kwa serikali kuu, kizuizi cha shughuli za biashara, kufungia shughuli za uwekezaji au ubatilishaji wa vibali vya uwekezaji, iwapo kwa wawekezaji ambao wanashindwa kuzingatia mahitaji yote yaliyoainishwa katika Sheria ya Uwekezaji ikiwa ni pamoja na shughuli za CSR.[260]

### 5.9 Hitimisho

Kwa kuangalia sheria za nchi mbalimbali, ni wazi kwamba dhana mbili ambazo ni Utawala Bora na Jukumu la kuwajibika kwa jamii zimeainishwa vyema. Sheria hizo zinajumuisha masuala ya misaada na huduma za jamii, masuala ya mazingira, ajira, ulinzi wa watoto na wanawake, watu wenye ulemavu, na jumuiya nyenginezo, katika kusimamia mambo ya uendeshaji wa kampuni.

Aidha uzoefu unaonesha kuimarishwa majukumu ya taasisi, wawekezaji na Kampuni kwa jamii kwa ujumla na kutekeleza taratibu sahihi za kukabiliana na matatizo kadhaa ambayo jamii inaweza kukutana nayo kutokana na shughuli za Kampuni, mwekezaji, taasisi au vyenginevyo.

Hata hivyo, bado kuna changamoto nyingi zinazokabili utekelezaji huo kama vile kukosekana sera na miongozo maalum; ukosefu wa uwazi na uhaba wa rasilimali za kifedha, tuhuma za rushwa, adhabu za wazi kwa kutokuwajibika n.k.

[260] Kifungu cha 33

Kwa upande wa sheria za CSR, ni dhahiri kwamba serikali zimeweka sheria za kutawala makampuni kuhusu CSR. Hata hivyo, ukosefu wa  wazi wa adhabu, katika sheria inadhoofisha utekelezaji wa sheria hizi.

# SURA YA SITA

## 6.0 MATOKEO YA UTAFITI

### 6.1 Njia zilizotumika katika Utafiti

Njia zilizotumika kufanyia tafiti eneo la usimamizi wa wajibu wa kutoa huduma kwa j amii (CSR), Tume imehusisha utafiti wa ndani uliopitia sera, sheria mbalimbali, mikataba ya kimataifa, vitabu na maandiko mbalimbali yaliyozungumzia Wajibu wa kutoa huduma kwa jamii (CSR).

Aidha njia nyengine ni kukutana na wadau wanaohusika na eneo hili wakiwemo wawekezaji, kampuni, taasisi, halmashauri, wananchi na wadau wengine kwa upande wa Unguja na Pemba.

### 6.2 Uchambuzi wa wadau

Wadau waliohusishwa katika utafiti huu walikusanywa kutoka taasisi mbalimbali zinazohusika katika utoaji huduma kwa jamii kama ifuatavyo:

1. OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora
2. Wizara ya Utalii na mambo ya Kale
3. Kamisheni ya Utalii
4. Mamlaka ya Kukuza naKulinda Uwekezaji
5. Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira
6. Chama cha Wafanya biashara

7. Ofisi ya Msajili wa Hazina
8. Jumuiya ya Wawekezaji Sekta ya Utalii
9. Baraza la Manispaa Magharibi A
10. Baraza la Manispaa Magharibi B
11. Baraza la Manispaa Mjini
12. Baraza la Mji Kaskazini A
13. Baraza la Mji Kaskazini B
14. Halmashauri Wilaya ya Kusini Unguja
15. Baraza la Mji Chake Chake
16. Baraza la Mji Wete
17. Baraza la Mji Mkoani
18. Halmashauri Wilaya ya Micheweni
19. kampuni za Uwekezaji
20. Masheha
21. Madiwani

## 6.3 Sampuli za utafiti

Kufikia malengo ya utafiti huu, jumla ya makundi ishirini na moja (21) yalihusishwa. Makundi hayo yalijumuisha Taasisi mbalimbali za Serikali, na Taasisi za binafsi na taasisi zinazosimamia wawekezaji na kampuni zinazohusiana na utoaji wa huduma za kijamii.

Vikao vya wadau vilifanyika katika maeneo tofauti ya Zanzibar. Jumla ya wawakilishi wote walioshirikishwa ni 83. Katika idadi hii ya washiriki, wanawake walikuwa ni 31 na wanaume walikuwa ni 62.

***Jadueli Nam. 1: idadi ya washiriki wote***

| Makundi | Waliohudhuria | Walioalikwa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora | 4 | 4 | 100.0 |
| Wizara ya Utalii na mambo ya Kale | 4 | 4 | 100.0 |
| Kamisheni ya Utalii | 4 | 4 | 100.0 |
| Mamlaka ya Kukuza naKulinda Uwekezaji | 4 | 4 | 100.0 |
| Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira | 4 | 4 | 100.0 |
| Chama cha Wafanya biashara | 4 | 4 | 100.0 |
| Msajili wa Hazina | 4 | 4 | 100.0 |
| Jumuiya ya Wawekezaji Sekta ya Utalii | 6 | 6 | 100.0 |
| Baraza la Manispaa Magharibi A | 3 | 4 | 75.0 |
| Baraza la Manispaa Magharibi B | 3 | 3 | 100.0 |
| Baraza la Manispaa Mjini | 3 | 4 | 75.0 |
| Baraza la Mji Kaskazini A | 3 | 3 | 100.0 |
| Baraza la Mji Kaskazini B | 3 | 4 | 75.0 |
| Halmashauri Wilaya ya Kusini Unguja | 2 | 2 | 100.0 |
| Baraza la Mji Chake Chake | 3 | 4 | 100.0 |
| Baraza la Mji Wete | 4 | 4 | 100.0 |
| Baraza la Mji Mkoani | 4 | 6 | 100.0 |
| Halmashauri Wilaya ya Micheweni | 4 | 6 | 100.0 |
| Makampuni za Uwekezaji | 9 | 10 | 90.0 |
| Masheha | 4 | 4 | 100.0 |
| Madiwani | 4 | 4 | 100.0 |
| | **83** | **92** | **90.2** |

***Jadueli Nam. 2: idadi ya washiriki wote Unguja***

| Makundi | Waliohudhuria | Walioalikwa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora | 2 | 2 | 100.0 |
| Wizara ya Utalii na mambo ya Kale | 2 | 2 | 100.0 |
| Kamisheni ya Utalii | 2 | 2 | 100.0 |
| Mamlaka ya Kukuza naKulinda Uwekezaji | 2 | 2 | 100.0 |
| Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira | 2 | 2 | 100.0 |
| Chama cha Wafanya biashara | 2 | 2 | 100.0 |
| Msajili wa Hazina | 2 | 2 | 100.0 |
| Jumuiya ya Wawekezaji Sekta ya Utalii | 4 | 4 | 100.0 |
| Baraza la Manispaa Magharibi A | 3 | 4 | 75.0 |
| Baraza la Manispaa Magharibi B | 3 | 3 | 100.0 |
| Baraza la Manispaa Mjini | 3 | 4 | 75.0 |
| Baraza la Mji Kaskazini A | 3 | 3 | 100.0 |
| Baraza la Mji Kaskazini B | 3 | 4 | 75.0 |
| Halmashauri Wilaya ya Kusini Unguja | 2 | 2 | 100.0 |
| Makampuni za Uwekezaji | 9 | 10 | 90.00 |
| Masheha | 2 | 2 | 100 |
| Madiwani | 2 | 2 | 100 |
| | **48** | **52** | **92.31** |

***Jadueli Nam. 3: idadi ya washiriki wote Pemba***

| Makundi | Waliohudhuria | Walioalikwa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora | 2 | 2 | 100.0 |
| Wizara ya Utalii na mambo ya Kale | 2 | 2 | 100.0 |
| Kamisheni ya Utalii | 2 | 2 | 100.0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mamlaka ya Kukuza naKulinda Uwekezaji | 2 | 2 | 100.0 |
| Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira | 2 | 2 | 100.0 |
| Chama cha Wafanya biashara | 2 | 2 | 100.0 |
| Msajili wa Hazina | 2 | 2 | 100.0 |
| Jumuiya ya Wawekezaji Sekta ya Utalii | 2 | 2 | 100.0 |
| Baraza la Mji Chake Chake | 3 | 4 | 75.0 |
| Baraza la Mji Wete | 4 | 4 | 100.0 |
| Baraza la Mji Mkoani | 4 | 6 | 66.7 |
| Halmashauri Wilaya ya Micheweni | 4 | 6 | 66.7 |
| Masheha | 2 | 2 | 100.0 |
| Madiwani | 2 | 2 | 100.0 |
| | **35** | **40** | **87.5** |

***Chati Nam. 1: Idadi ya washiriki wote kiasilimia***




***Chati Nam. 2: Idadi ya washiriki wote kiasilimia***


Asilimia ya Washiriki Kijinsia - Unguja
35.4
64.6
Wanaume
Wanawake


Asilimia ya Washiriki Kijinsia - Pemba
37.1
62.9
Wanau
me


Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu - Zanzibar
14.5
12
38.6
32
39
47.0
Elimu ya Sekondari
Elimu Baada ya Sekondari


Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu - Unguja
12.5
6
39.6
19
23
47.9
Elimu ya Sekondari


Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu - Pemba
17.1
6
37.1
13
16
45.7
Elimu ya Sekondari
Elimu Baada ya Sekondari


Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Umri - Zanzibar
16.9
19.3
14
16
53
63.9
A (15 - 24)
B (25- 60)


Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Umri - Unguja
16.7
18.8
8
9
31
64.6
A (15 - 24)
B (25- 60)
C (60+)


Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Umri - Pemba
17.1
20.0
6
7
22
62.9
A (15 - 24)
B (25- 60)

### 6.4 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanatokana na sehemu kubwa ya njia za utafiti ambazo zimetumika kukamilisha utafiti huu. Njia hizo zilijumuisha upitiaji wa sera, sheria mbali mbali za Zanzibar, mipango ya Taifa, mikataba ya kimataifa, uzoefu wa nchi mbali mbali, fasihi zinazohusiana na suala la uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii na maoni ya wadau walioshiriki katika kutoa maoni yao kuhusiana na utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha yaliyojitokeza yakiwemo masuala ya kisheria na masuala ya kiutendaji. Matokeo hayo yanaelezewa kwa kina hapa chini kama ifuatavyo.

#### (a) Mfumo wa kisheria kusimamia Uwajibikaji wa Wawekezaji

Utafiti umebaini kuwa kwa sasa Zanzibar haina mfumo wowote wa kisheria katika kusimamia suala la uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii. Baada ya kupitia mfumo wa sera na sharia, imebainika kwamba hakuna sharia yoyote inayoweka wajibu wa moja kwa moja kwa wawekezaji kwa ujumla kuwajibika kwa jamii zinazozunguka uwekezaji huo. Utafiti wetu umebaini kuwa baadhi ya sheria zimeweka aina Fulani za wajibu wa wawekezaji kwa jamii ikiwemo wajibu wa kutunza mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira, wajibu kwa makampuni ya uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na maeneo mengine machache.

Pamoja na kuwepo kwa sharia hizo chache katika baadhi ya maeneo, hata hivyo, sharia hizo hazikuweka mfumo mzuri wa usimamizi wa uwajibikaji huo hasa kukosekana kwa kwa masharti ya tathmini na kutilia nguvu, pale inapotokea mwekezaji kutotimiza wajibu huo.

Kwa msingi wa matokeo haya, Tume imebaini pengo liliopo na haja ya kuwepo kwa mfumo wa kisheria utakaosimamia suala hili la uwajibikaji wa wawekezaji kwa ujumla, mbele ya jamii.

**(b) Kutungwa kwa Sheria mahsusi ya Wajibu wa Wawekezeji**

Pamoja na utafiti wetu kubaini kuwa nchi nyingi zimeweka wajibu wa wawekezaji kuwajibika kwa jamii katika sharia za makampuni, tumebaini kuwepo kwa sharia mahsusi katika baadhi ya nchi, zinazosimamia moja kwa moja suala la wajibu wa wawekezaji kwa jamii. Kwa msingi huo, utafiti huu unadhihirisha kuwa utungaji wa sharia mahsusi katika eneo hilo si jambo jipya na uwajibikaji huo unaweza kusimamiwa vizuri zaidi kwa uwepo wa sharia mahsusi kama hiyo.

**(c) Wawekezaji wanaostahiki kuwajibika kwa jamii**

Utafiti huu umebaini kuwa, pamoja na kuwepo kwa tofauti katika kuamua mwekezaji wa aina gani anapaswa kuwajibika kwa jamii kutokana na uzoefu wa nchi mbali mbali, jambo la msingi ni kuwa si wawekezaji wa aina na viwango vyote ambao watawajibika kwa jamii. Utafiti huu umebaini kuwa baadhi ya nchi zimekuwa zikibainisha aina ya makundi maalum ya wawekezaji ambayo yatalazimika kuwajibika kwa jamii na si kila mwekezaji hasa kutokana na uataratibu wa kuwabana na kuwasimamia wawekezaji katika kuhakikisha kuwa wanatekeleza wajibu wao kwa jamii.

**(d) Usimamizi wa uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii**

Utafiti umebaini kuwa uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii uliobainishwa katika baadhi ya sharia ikiwemo sharia ya mafuta na gesi asilia na sharia

nyenginezo, hautekelezwi ipasavyo kutokana na sharia kutobainisha kwa uwazi, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa wajibu huo. Kwa msingi huo, wawekezaji wengi wamekuwa wakichukulia suala la kutoa na kurejesha faida kwa jamii zinazonguka uwekezaji ni suala la khiyari kwa kuwa hakuna mfumo wa kusimamia kisheria utekelezaji wa Sheria hii.

Katika utafiti huu tumebaini kuwa baadhi ya nchi zimeweka utaratibu wa kisheria wa kusimamia uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii. Kwa utaratibu huo, wawekezaji wamekuwa wakilazimika kutekeleza wajibu wao kwa jamii kwa kuwa sharia zimeweka taratibu nzuri za kusimamia na kutathmini namna wajibu huo ulivyotekelezwa. Aidha, utafiti wetu umegundua kuwa baadhi ya nchi zimeweka hata adhabu kwa wawekezaji wanaoshindwa kutekeleza masharti ya kisheria ya kuwajibika kwa jamii.

### (e) Wawekezaji kuripoti utekelezaji wa wajibu wao kwa jamii

Eneo jengine ambalo utafiti huu umebaini ni suala la kuwepo kwa utaratibu wa kisheria wa kuwataka wawekezaji husika kuripoti namna walivyotekeleza wajibu wao kwa jamii. Tume imegundua kuwa utaratibu huu wa kuripoti utekelezaji kuwekewa msingi wa kisheria, kunasaidia utekeleaji huo wa wajibu wa wawekezaji kwa kuchelea kuonekana dhahiri kushindwa kuripoti utekelezaji wao wa namna ilivyotekeleza wajibu wao kwa jamii. Imebainika kuwa utaratibu huo wa kuripoti namna wawekezaji walivyotekeleza wajibu wao kwa jamii umekuwa ukitumika katika nchi mbali mbali na kipindi cha kuripoti ni kwa kila mwaka.

### (f) Vyanzo vya fedha katika kutekeleza wajibu wa wawekezaji kwa Jamii

Katika utafiti huu, Tume imebaini kuwa miongoni mwa mambo muhimu ya kuzingatiwa katika utekelezaji wa wajibu wa wawekezaji kwa jamii ni pamoja na kuwekwa wazi vyanzo vya fedha vitakavyotumika kugharamia utekelezaji hu. Mifumo ya sharia ya nchi mbali mbali imeweka wazi ndani ya sharia hizo kuwa, gharama za utekelezaji wa wajibu wa wawekezaji kwa jamii zitatokana na fedha za taasisi hizo za wawekezaji au sehemu ya faida inayozalishwa na wawekezaji hao. Utafiti wetu haukubaini kuwepo kwa Mifuko iliyoanzishwa na serikali za nchi kugharamia utekelezaji huo wa wawekezaji kwa jamii.

### (g) Chombo maalum cha kuratibu na kusimamia utekelezaji wa wajibu wa wawekezaji kwa jamii

Utafiti huu umebaini kuwa utekelezaji wa wajibu wa wawekezaji kwa jamii unaweza kutekelezwa vyema pale panapokuwa na chombo au taasisi maalum ya utekelezaji wa wajibu huo. Baada ya kupitia sharia mbali mbali za Zanzibar ambazo kwa kiasi fulani zimeweka wajibu huo kwa wawekezaji, tumebaini kutokuwepo kwa ufanisi katika utekelezaji huo kutokana na kukosekana kwa chombo maalum kilichopewa mamlaka ya kisheria kusimamia na kuratibu suala hilo. Utafiti umebaini kuwa chombo hicho cha usimamizi na uratibu wa wajibu wa wawekezaji kinaweza kuwa chombo kipya au taasisi ziliopo katika muundo wa Serikali kupewa mamlaka ya usimamizi wa eneo hilo.

### (h) Suala la mazingira na ajira kujumuishwa katika uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii

Utafiti huu umebaini kuwa suala la uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii halihusu utoaji wa fedha kugharamia miradi ya kijamii pekee, bali ni suala linalohusisha pia wajibu wa wawekezaji hao kushiriki katika kutunza mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na baadae. Hivyo, uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii unahusisha wawekezaji hao katika shughuli zao kuhakikisha kuwa wanahifadhi mazingira na miradi yao haichangii katika uharibifu wa mazingira. Utafiti huu umebaini kuwa hakuna utaratibu madhubuti wa wawekezaji wanaochangia uharibifu wa mazingira kulipa fidia ambayo itawanufaisha wananchi watakaoathirika moja kwa moja na madhara yatakayojitokeza kutokana na uchafuzi huo wa mazingira, na fidia hiyo itatumika katika kuwapatia kinga mbadala wananchi hao au kutumika katika kuyarejesha katika hali ya awali maeneo yaliyoathirika.

Utafiti huu pia umebaini kuwa uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii unahusisha suala la wawekezaji kutoa ajira kwa wananchi hasa wa maeneo yanayozunguka miradi ya wawekezaji hao. Pamoja na dhana ya uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii kuhitaji uzingatiaji wa ajira kwa wananchi, kwa upande wa Zanzibar, utafiti wetu umebaini kutofanyiwa kazi ipasavyo kwa suala hili hata kwa sekta zilizoelekezwa kutekelezwa kwa hatua hiyo ya kuwaaji wananchi katika miradi hiyo ya kiuwekezaji. Aidha, utafiti umebaini udhaifu katika eneo hilo kwa hilo la ajira kwa wageni wengi kupatiwa ajira kwa kazi ambazo zingeweza kufanywa na wazanzibari na kumekuwa na malalamiko mengi katika suala hilo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti wetu, kumekuwa na uelewa finyu wa jamii kuhusu dhana hii ya uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii, kwa kuamini kuwa

dhana hii inahusisha fedha za miradi ya kijamii kama vile ujenzi wa skuli, vituo vya afya, visima vya maji na miradi mengine kama hiyo.

### (i) Uwelewa wa wajibu wa Wawekezaji kwa jamii

Kupitia vikao vya wadau vilivyofanyika wakati wa utafiti wa eneo hili, Tume imebaini kuwa wananchi wengi hawana uelewa kuhusu suala hili la wajibu wa wawekezaji kwa jamii. Miongoni mwa watu ambao utafiti umebaini kuwa hawana uelewa wa kutosha kuhusu wajibu huo wa wawekezaji kwa jamii ni pamoja na masheha, wana asasi za kiraia na maafisa wa halmashauri za wilaya, watu ambao walipaswa kuwa na uelewa mkubwa zaidi wa suala hilo kutokana na nafasi zao katika maendeleo ya nchi kwenye jamii zao.

Tume imebaini kuwa hakuna elimu ya kutosha miongoni mwa makundi mbali mbali ya wanajamii na hata wawekezaji kuhusu wajibu wa wawekezaji kwa jamii. Utafiti huu umebaini kuwa uelewa huo ni mdogo hata kwa sharia zilizoweka wajibu huo kama vile Sheria ya Utalii na Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia.

Shughuli za kujumuishwa katika uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii

Tume imebaini kuwa suala la uwajibikaji wa wawekezaji kwa jamii limekuwa likibainishwa kwa uwazi kwa kueleza maeneo mahsusi ambayo uwajibikaji kwa jamii unaweza kufanywa ili kuepuka uwajibikaji huo kufanyika katika maeneo ambayo hayatonufaisha jamii kwa ujumla. Miongoni mwa shughuli hizo za kuzingatiwa

# SURA YA SABA

## 7.0 MAPENDEKEZO YA TUME NA HITIMISHO

## 7.1 Utangulizi

Sehemu hii inaeleza mapendekezo ya Tume ya Kurekebisha sheria katika uanzishwaji wa utaratibu maalum kisheria juu ya wajibu wa kuwajibika kwa jamii. Wajibu huu kutokana na utafiti uliofanywa unajumuisha kampuni, wawekezaj, mashirika ya Umma na wadau wengine ambao wana wajibu wa kutoa michango yao kwa jamii na kuendeleza uchumi wa nchi.

Baada ya kufanya Utafiti huu, kwa kuangalia sheria zetu za ndani zinazosimamia masuala ya uwekezaji na wajibu wa wawekezaji, kuangalia uzoefu wa Sheria za Nchi mbalimbali, matakwa ya Mikataba ya Kimataifa na Kikanda, Sera na miongozo ya nchi ikiwemo Dira 2050, Ilani ya CCM na MKUZA III, mapitio ya rejea na maoni ya wadau Unguja na Pemba, Tume inapendekeza yafuatayo:

## 7.2 Mapendekezo ya Kisheria

### (a) Kuanzishwa kwa Sheria

Tume inapendekeza kuanzishwa kwa sheria ya Uwajibikaji kwa Jamii kwa lengo la kuratibu vizuri wajibu wa Makampuni, taasisi na vyombo vyengine vinavyotakiwa kutoa huduma kwa jamii zinazowazunguka. Aidha, suala la uwajibikaji kwa jamii limeelezwa katika sheria mbali mbali hivyo, ni vyema kuwa na sheria maalum itakayoweka masharti na usimamizi wa huduma kwa jamii.

### (b) Mazingatio ya Sheria

Tume inapendekeza sheria izingatie yafuatayo:

(i) Misingi ya CSR itakayojumuisha maeneo ya kupatiwa huduma au miradi, na kutoa fursa kwa kila taasisi kuchangia katika maendeleo ya wananchi kwa kutokana na faida inayopatikana.

(ii) Kutaja maeneo yatayohusika katika CSR kama vile eneo la misaada; masuala ya kisayansi; maendeleo ya vijana na michezo; masuala ya kitamaduni au elimu; huduma kwa wastaafu na wazee; ustawi wa jamii; uendelevu wa mazingira; afya; na msaada na usaidizi wakati wa maafa.

(iii) Upeo wa watoa huduma za CSR kama vile wawekezaji, kampuni, taasisi za umma zinazotengeneza faida, Asasi za kiraia nk.

(iv) Jukumu la Serikali ikiwemo kutambua na kuheshimu mchango wa taasisi binafsi na za Serikali katika eneo la CSR na kusaidia na kuratibu utekelezwaji wa miradi au huduma inayotolewa kwa jamii katika utaratibu wa CSR.

(v) Jukumu la watoa huduma za CSR ikiwemo kutekeleza sheria, kuweka sera za utekelezaji wa CSR na kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya CSR.

(vi) Kuanzishwa kwa jukwaa la watoa huduma ambalo litajumuisha wajumbe kutoka sekta mbalimbali katika utekelezaji wa CSR.

(vii) Majukumu ya jukwaa la watoa huduma ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya miradi ya huduma zilizotolewa na kuishauri Serikali juu ya utekelezaji mzuri wa CSR.

(viii) Sheria kuruhusu utekelezaji wa pamoja wa miradi ys CSR kupitia miongozo maalum.

(ix) Uwasilishaji wa ripoti za utekelezaji wa wajibu wa CSR kila mwaka.

(x) Makosa na adhabu.

**(c) Utolewaji wa elimu.**

Tume inapendekeza sheria iweke utaratibu wa kutolewa elimu kwa watoa huduma ikiwemo wawekezaji, kamouni na taasisi nyengine zilizotajwa kiseria kwa upande mmoja na wananchi kwa ujumla. Hatua hii itatoa uelewa wa dhana nzima ya CSR na kuisaidia Serikali katika utekelezaji wake. Aidha, Tume inapendekeza Taasisi za Serikali kupatiwa elimu na kueleweshwa wajibu wao katika CSR.

**(d) Usimamizi wa CSR**

CSR ni eneo la msingi katika utekelezaji wa utawala bora na misingi ya uwajibikaji inataka kamouni, wawekezaji na taasisis zinazotengeneza faida kuchangia katika maendeleo ya jamii. Kutokana na msingi huo, Tume inapendekeza usimamizi wa CSR uwachwe chini ya Ofisi ya Rais, Katiba Sheria na Utawala Bora.

**(e) Kuoanisha masharti ya sheria nyengine na sheria ya CSR.**

Ili sheria hii iweze kutekelezeka vizuri, Tume inapendekeza Sheria zilizogusa na kuweka masharti ya CSR kama Sheria ya Uwekezaji Nam. 14 ya 2018, Sheria ya Mafuta na Gesi Nam. 6 ya 2016, Sheria ya Utalii Nam.6 ya 2019, Sheria ya Kampuni Nam.15 ya 2013, Sheria ya PPP Nam.8 ya 2015, Sheria ya Mazingira Nam.3 ya 2015, Ofisi ya Msajili wa Hazina Nam. 6 ya 2021, Tawala za Mikoa Nam. 8 ya 2014 zizingatiwe ili zibaki na jukumu la kusaidia utekelezaji wa CSR.

### 7.3 Mapendekezo ya Kiutendaji

Kwa upande wa mapendekezo ya kiutendaji tume imepokea mapendekezo yafuatayo kutoka katika vikao mbali mbali vya wadau:

#### (a) Ushirikiano baina ya taasisi

Tume inapendekeza katika kutekeleza uwajibikaji kwa jamii, Serikali iweke utaratibu maalum na kuratibu ushirikiano baina ya taasisi na mamlaka zote ambazo zitakuwa na wajibu kwa namna moja ama nyengine katika masuala ya uwekezaji kuanzia ngani za chini katika Shehia mpaka Serikali kuu.

#### (b) Kuhamasisha wananchi kuunga mkono CSR

Tume inapendekeza Serikali kuchukua jitihada za kuhamasisha wananchi kuunga mkono juhudi zinazochukuliwa na makampuni, wawekezaji na taasisi zinazoingiza faida katika kuisaidia jamii kupitia CSR.

#### (c) Kusimamia matumizi sahihi ya fedha zinazotokana na CSR.

Tume inapendekeza vyombo husika vya Serikali kusimamia matumizi ya fedha zitakazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali ya CSR.

### 7.4 Hitimisho

Kutungwa kwa Sheria ya Wajibu wa Wawekezaji kwa Jamii kutasaidia kuweka utaratibu maalum wa utekelezaji wa miradi ya kijamii inayotokana na sehemu ya faida zitokanazo na uwekezaji wa wafanya biashara nchini, lakini pia kuweka misingi ya kisheria ya kudhibiti pamoja na kukabiliana na athari za kimazingira zitokanazo na uwekezaji. Aidha hatua hii itatekeleza kwa vitendo mipango ya Serikali ya kupunguza umasikini na kuchochea maendeleo ya wanajamii na

wazanzibari kwa ujumla kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo 2050. Mara baada ya sheria kupitishwa, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inatarajia kuwa ni sehemu ya hatua kubwa za kupunguza umasikini na kuchochea ukuaji wa uchumi hasa kwa wananchi wa kipato cha chini na cha kati pamoja na ustawi wa jamii na wanajamii kwa ujumla.

Kwa hivyo, msukumo wa kuanzishwa Sheria hii kwa kiasi kikubwa utasaidia utekelezaji wa wajibu wa wawekezaji katika kuzisaidia jamii za wazanzibari hususani katika jamii ambazo zinakabiliwa na athari za uwekezaji unaofanywa katika sehemu husika kwa kutekeleza matakwa ya kisheria kutatua mahitaji ya wanajamii hao katika maeneo ya miradi itakayopendekezwa na kwa muda mahususi na kiwango maalum kulingana na ukubwa wa faida inayopatikana katika uwekezaji husika.

**THE ZANZIBAR CORPORATE SOCIAL RESPONSIBILITIES ACT**

| | |
|---|---|
| Short Title | 1. This Act shall be known as the "Corporate Social Responsibility Act". |
| Interpretation | 2. Jj<br><br>"corporate social responsibility" refers to the commitment of business to behave ethically and to contribute to sustainable economic . development by working with relevant stakeholders to improve their lives in ways that are good for business, sustainable development agenda and society at large<br><br>Responsible authority<br>Sector authority<br>Corporate social responsibility<br>Government |
| Principles of CSR | 3. The CSR shall be governed by the following principles:<br>(a) the company shall give preference to the local area and areas around it where it operates, for spending the amount earmarked for Corporate Social Responsibility activities |

| | |
|---|---|
| | (b) All stakeholder shall contribute in economic development<br>(c) Kuhakikisha wadau wote wanafahamishwa kikamilifu kuhusu shughuli za Wajibu wa Wawekezaji kwa Jamii<br>(d) the Governments shall encourage its active, participation in fostering sustainable economic development and environment protection in the Zanzibar |
| Corporate social responsibility activity | 4. CSR related activities shall include, but not be limited to the following:<br><br>(a) Charitable;<br>(b) Scientific;<br>(c) Youth and sports development;<br>(d) Cultural or educational purpose;<br>(e) Services to veterans and senior citizens;<br>(f) Social welfare;<br>(g) Environmental sustainability;<br>(h) Health; and<br>(i) Disaster relief and assistance.<br>Provided, these CSR activities shall exclude mandatory activities already imposed upon company, institution or organisation as provided by existing Zanzibar legislations. |

| | |
|---|---|
| Scope of Corporate Social Responsibility | 5. Any corporation, whether domestic or foreign, partnerships and other establishments performing business in the country are hereby mandated to observe its corporate social responsibility or the obligation to consider the interests of society by taking responsibility for the impact of their activities on customers, employees, shareholders, communities and the environment in all aspects of their operations. |
| Role of Government in CSR | 6. The Government shall have the following roles:<br><br>(a) the Government to recognize the vital role of the private and public sectors in nation building<br>(b) the Governments shall encourage its active, participation in fostering sustainable economic development and environment protection in the Zanzibar.<br>(c) the Government, shall coordinate its various agencies and non -government organization to work hand in hand for the integration, promotion, and strengthening of corporate social responsibility in all business organization. |
| | |
| Role | 7. Any company, investor, institution and any other organization which is capable for investment or |

| | |
|---|---|
| of investors, organisation, companies, public institution etc | required to comply with corporate social responsibility law shall:<br>(a) Generate profit to comply with a Corporate Social Responsibility Plan<br><br>(b) disclose the plan of the Corporate Social Responsibility responsible authorities.<br><br>(c) formulate Social Responsibility Policy which shall indicate the activities to be undertaken by the company, organisation or institution<br><br>(d) recommend the amount of expenditure to be incurred on the activities referred to in clause (a); and (c)<br><br>(e) monitor the Corporate Social Responsibility Policy of the company from time to time.<br><br>(f) ensure that the activities as are included in Corporate Social Responsibility Policy of the company are undertaken by the company<br>(g) ensure that the company spends, in every financial year, at least two per cent of the average net profits of the company made during the three immediately preceding financial years, in |

| | |
|---|---|
| | pursuance of its Corporate Social Responsibility Policy: |
| The Corporate Social Responsibility Forum | 8. lt is hereby established a forum to be known as the Corporate Social Responsibility Forum which shall constitute ten representative members from:<br>(a) companies<br>(b) public institution<br>(c) non-governmental organisations<br>(d) 3 investors from prime sectors in Zanzibar<br>(e) Director of Good governance<br>(f) |
| Duties of the Forum | 9. The forum shall have the following duties:<br>(a) to receive and assess general reports and performance of CSR activities in Zanzibar<br>(b) advice the government on the areas to be considered in CSR activities<br>(c) receive any complain form investor, company or any orgamnisation in the performance of social corporate responsibility project or any area specified in this Act<br>(d) …….. |
| Joint Corporates Responsibilities | 10. The companies, organizations, institutions shall be allowed to have jointly corporate responsibility in the same local area, if the projects will be well performance in jointly efforts basis |

| | |
|---|---|
| Periodic Report. | 11. (1) All companies, institution and any other organization shall submit their annual report of activities relative to their corporate social responsibility not later than January 31 of each year.<br>(2) the report shall be submitted to responsible authority and the sector authority |
| Implementing Rules and Regulations | 12. All government institutions and local authority institutions shall, promulgate rules and regulates for the effective implementation of this Act and shall regularly monitor strict compliance therewith. |
| **Offences** | 13. If the company, institution or organisation fails to spend such amount, as provided under this Act, shall, specify the reasons for not spending the amount.<br><br>Fails to comply |
| Repealing Clause | 14. All laws, decrees, orders, rules and regulations, and other issuances, or parts thereof, inconsistent with this Act are hereby repealed or modified accordingly. |

**SCHEDULE**

**PROGRAMS OR ACTIVITIES RELATING TO CSR**

| NO: | ACTIVITY |
|---|---|
| 1. | Eradicating poverty, hunger and malnutrition and promoting health care. |
| 2. | Improvement in education which includes special education and employment strengthening vocation skills among children and women. |
| 3. | Improving gender equality, setting up homes and hostels for women orphans and old age homes. |
| 4. | Safeguarding environmental sustainability, ecological balance, protection of flora and fauna, animal welfare, agroforestry, conservation of natural resources and maintaining a quality of soil, air and water. |
| 5. | Protection of national heritage, art and culture including restoration of buildings and sites of historical importance and works of art; setting up public libraries; promotion and development of traditional arts and handicrafts. |
| 6. | Measures for the benefit of widows and their dependents. |
| 7. | Training to stimulate rural sports, nationally recognized sports. |

| | |
|---|---|
| **8.** | Contribution to research and development projects in the field of science, technology, laws, engineering and medicine. |
| **9.** | Infrastructures |